Nenda, Kamwamshe Yesu

Bwana, naamini,
Mambo yote yawezekana, Bwana, naamini.

2 Na tuendelee kusimama kwa muda mfupi tu, kwa ajili ya maombi. Na wakati tukiinamisha vichwa vyetu sasa, sijui, katika kusanyiko hapa, na katika orofa ya chini, kama kulikuwa . . . na juu kwenye roshani, popote pale, iwapo mtu yeyote katika Uwepo wa Kiungu angetaka ijulikane usiku wa leo mbele za Mungu, katika haja maalum, naomba uinue tu mkono wako Kwake sasa. Na ushikilie wazo lako sasa na kile unachowazia, na uamini tu kwamba Kristo amesimama moja kwa moja mbele zako.

3 Baba wa Mbinguni, tumesimama hapa huku tumeinua mikono yetu, na, kama ndugu alivyosema, "Ni ishara ya watu wote ya kujisalimisha." Nasi tunajisalimisha Kwako, kama mabonge ya towe yaliyotoka ardhini, nasi tunaomba, Mungu, kwamba Wewe utawajaza usiku wa leo na Roho Wako na Uzima, na ujitwalie Mwenyewe utukufu. Nena kupitia sisi, usiku wa leo. Fanya kazi kupitia sisi, kwa utukufu Wako. Jibu kila haja, Bwana. Unazijua zote. Unajua kilichoko nyuma ya mikono yetu, na nia zetu, malengo yetu, na kile tunachohitaji, na ninii . . . kile tungefanya nacho kama tungekipata. Pia, Bwana, ninaomba ya kwamba utaisafisha mioyo yetu, na mawazo, na nia, kwamba ikiwa tutapokea kile tunachoomba, kiwe ni kwa heshima Yako. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu, tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

4 Ni vyema kurudi katika nyumba ya Bwana, usiku wa leo. Ninaweza kujisikia kuzuiliwa kidogo tu. Shetani amekuwa akijaribu kunikabidhi mafua mabaya, kila tangu New York. Na kila mara anaponikabidhi hayo, ninayarudisha moja kwa moja kwake; naye ananikabidhi, na kisha ninayarudisha moja kwa moja kwake, unaona. Kwa hiyo kwa namna fulani tunasumbuana juu ya hayo, kwa hiyo ninajua Bwana ataingilia baada ya kitambo kidogo na kuchukua upande mmoja. Basi kwa hiyo . . .

5 Nami ninaomba ya kwamba Bwana atawajalia haja zenu zote, usiku wa leo. Sasa tumeutoa usiku wa leo kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Sasa, nadhani wengi wenu mnashangaa, mara nyingi, katika kuja kuivuka nchi, wao . . . Ninatangaza ninaenda kuwa na mkutano, wazo la kwanza ni uponyaji wa Kiungu, unaona.

6 Ila, kuna mengi zaidi kwa huduma mbali na uponyaji wa Kiungu, mnaona. Mwili ulio mgonjwa kuliko yote nijuayo, usiku

wa leo, ni ule unaoitwa Mwili wa Yesu Kristo. Unahitaji uponyaji wa kiroho. Kuna dawa moja tu ninayojua itakayoponya, na hiyo ni Neno. Na huo ndio Mwili mgonjwa ambao tunataka kusimama katika uweza na nguvu za vitamini ya Injili. Na hiyo ndiyo sababu ninatumia muda mwingi sasa katika kujaribu kulitia nguvu Kanisa, kwa Neno.

7 Ninajua mimi ni mbadala hafifu kuchukua mahali pa mhudumu, mhudumu mwenye elimu. Ila ninaamini hili, bila madharau yoyote kwa—kwa huduma ya usomi. Laiti ningekuwa nayo. Na mimi sijaribu kutetea ujinga wangu, kwa kusema hili. Bali kile tunachohitaji sasa, zaidi ya tunavyohitaji upande wa kielimu kujua jinsi ya kuliweka Neno pamoja na kulifanya Hilo liingie sawasawa kwa uhodari, ni Mungu. Tunamhitaji Mungu. Mnaona? Mnaona? Na haliji kila mara kupitia maneno yaliyotungwa vizuri. Hu—huja kupitia moyo uliowekwa wakfu, na moyo huo uliowekwa wakfu kwa Mungu na kufanya mapenzi ya Mungu. Sasa, inakubidi kuyajua mapenzi kabla ya kuweza kuyatimiza hayo mapenzi. Tafuta kujua uko hapa kwa nini. Si tu kuninii . . .

8 Daima nimewazia kwamba Kanisa halikuwa ovyoovyo. Yesu kamwe hakuja duniani kwa njia ovyoovyo. Kamwe hakufa kwa njia ovyoovyo. Alikuja kwa kusudi, nalo kusudi hilo lilikuwa ni kutimiza Amri ya Mungu, ili aweze kujinunulia Mwenyewe Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi.

9 Kanisa hilo ni Kanisa lililochaguliwa kimbele. Kila jina lililowahi kuwekwa katika Kitabu hicho, Yesu alikuja kukomboa. Na wakati jina la mwisho limekombolewa, Kitabu kinafungwa. Sasa, Yeye hakukusudia kwamba hakuna mtu atakayepotea, bali kujua Kwake kimbele kulimfanya ajue ni nani atakayepotea. Hivyo basi, Yeye aliweza kuchagua kimbele, ndipo basi majina yao yakawekwa kwenye Kitabu. Na halafu wakati Kitabu hicho cha ukombozi kimefungwa na kutiwa muhuri kwa mihuri saba, wakati kinapotekelezwa na—na nguvu za ajabu za Mungu. Basi siku moja wakati Kitabu cha ukombozi kinapokamilika, Mwana-kondoo anakichukua. Ndipo basi jina la mwisho linaitwa kutoka kwa hicho, Mwana-kondoo anajitokeza kuita kile alichokomboa, hicho ni Kanisa Lake. Nami ninaamini wakati umekaribia.

10 Na sasa nimekuwa na nyakati ngumu sana za kufanya hili, na jambo moja, ni kujaribu kuiweka rekodi ya—yangu safi. Sasa, mara nyingi, nimekuwa na mara nyingi nimetangazwa na mahali ambapo si—sikuwa—sikuwahi kujua chochote kuhusu kuwa huko, na tangazo lisilo kweli. Chochote tu ambacho Shetani angeweza kunirushia, amefanya hivyo. Mtu fulani alikuja hivi majuzi, kasema, "Ninataka kujua kama hiyo ni kweli. Je! tutakuwa huko? Ni—ninataka tu kujua hilo." Unaona?

11 Sasa hapa hivi majuzi tu, nilitangazwa huko New York, sikujua chochote juu yake. Mmoja wa Wakristo Wafanyabiashara alimwambia mtu huyo nilikuwa niwe huko kwenye wakati huo, na alikuwa amemwambia ingekuwa sawa. Na hiyo—hiyo ilikuwa ni katika mwezi wa Oktoba, mkutano wao ulikuwa. Nami nilikuwa nimemwambia mtu huyu nilikuwa niwe huko Novemba, juma la kwanza katika Novemba, nilikuwa niwe New York, na ningezungumza katika mkutano wao kama ulikuwa ni wakati huo. Akasema, "Vema, huo ndio wakati utakaokuwapo." Lakini akasema Oktoba, mnaona, kitu hicho kidogo. Basi mtu yule huko New York, kabla ya kuuliza, kushauriana nasi, aliutangaza kote katika jimbo, mnaona, kuweko huko.

12 Majuma machache yaliyopita, kulikuwa na barua ya kueneza habari iliyosambazwa hapa katika Memphis, Tennessee, ilikuwa imetiwa sahihi na jina langu, nakala ya fotostat, na kusema nilikuwa na mtu huyu "kwa siku thelathini, katika kufunga." Siku tatu ndio muda mrefu zaidi niliowahi kufunga maishani mwangu. Mtu huyo, sikuwahi kusikia jina lake maishani mwangu; kasema nilitokeza na kufunga kutoka kwake, pamoja naye, hasa, na kasema kwamba nilikuwa niwe huko katika siku fulani, akawaambia marafiki zangu wote karibu na Memphis kuwepo kwenye mkutano huu fulani. Sikuwahi kusikia kuhusu mahali hapo, sikumjua mtu huyo, sikujua chochote kuhusu hilo, maishani mwangu; na sahihi bandia, iliyoigwa kwa udanyanyifu. Hata sitii sahihi jina langu; siamini mtu yeyote angeweza kuiga tena sahihi yangu, maana hata siijui baada ya kuiandika. Kwa hiyo, ni kitu kibaya tu hivyo, sioni jinsi ambavyo mtu yeyote anajaribu ku—anajaribu kufanya hilo.

13 Nilikuwa kwenye benki, hapa si muda mrefu uliopita. Inatubidi kuchukua hesabu ya kila kitu, kwa sababu ya sisi kuiweka sawa namna hiyo. Hundi iliyobatilishwa ndiyo—ndiyo risiti bora zaidi uwezayo kuwa nayo. Na sasa tumekuwa tukifanya hivyo sikuzote tangu tulipooana. Na kwa hiyo mtu wa benki akasema, "Siamini mtu yeyote angeweza kamwe kuiga sahihi hiyo, Bw. Branham."

14 Nikasema, "Vema, unajua, wanasema kila kitu hufanya kazi kwa wema."

15 Na kwa hiyo—na kwa hiyo, hapo, mambo hayo hulifanya gumu, huwafanya watu wafikirie kwamba unadanganya, wakati, si—sikujua chochote kuhusu kuwa huko. Na inaifanya basi, pasipo matangazo wala chochote, nimejaribu kuidumisha huduma yangu ambapo ningeweza kwenda popote ambapo Bwana aliniita. Sikuwa na wajibu kwa chochote au mtu yeyote ila Mungu, kudumu tu na Yeye.

16 Kusudi langu limekuwa, kanisani, ni kujaribu kuondolea mbali wazo hilo kutoka kwa hawa watu wa Amerika, kwamba lazima uwawekee mikono. Unaona? Nime—nime . . . Unapofanya hivyo, inaonekana kana kwamba wewe ni . . . Wanasema, "Vema, Ndugu *Nanii* alikuja, akaniwekea mikono." Mwache tu Yesu aweke mikono Yake juu yako, unaona, na imani yako iinuke na kumgusa Yeye. Lakini sasa nimekuwa na yapata miaka kumi na sita, na nimeshindwa nayo kabisa, unaona, wao . . . maana kuna wengi sana wanaotaka kuamini hili vinginevyo. Na kwa hiyo tunawaridhisha watu, tunalifanya kwa vyovyote vile, kuweka mikono juu yake.

17 Bali maoni yangu, kwamba ikiwa tunaweza kuona Uwepo na kujua kwamba Yesu Kristo yupo hapa, ni nini zaidi unachohitaji, wakati kusanyiko lote linaomba kwa wakati mmoja? Mnaona? Hapo ndipo nguvu za Bwana hushuka, wakati Neno linapojulikana. "Imani huja kwa kusikia, na kusikia Neno." Wakati Neno linapohubiriwa, Nalo ni Kweli, na Mungu akithibitisha Uwepo Wake, hilo—hilo linafaa kufanya kazi papo hapo.

18 Sasa, sasa, kesho asubuhi . . . Sasa, usiku wa leo, hasa, samahani, usiku wa leo nina somo fupi tu, kwa sababu tunaenda kuwaombea wagonjwa. Lakini kesho asubuhi, sasa, nafikiri ninapaswa kuwa na somo la shule ya Jumapili. Je! hiyo ni kweli? Lote litakuwa hapa katika ukumbi, nami nina so—so—somo ambalo ningependa, Bwana akipenda, lilikuwa . . . kama Yeye akinikubalia. Inanibidi kulisema hivyo, unaona. Nafikiri . . . ikiwa nyinyi—ikiwa nyinyi hamna shule yenu wenyewe ya Jumapili sasa. Ikiwa mna shule yenu wenyewe ya Jumapili, nenda kwenye shule yenu ya Jumapili. Ukitaka kusikia Hilo, wanazo kanda. Kwa hiyo ningekuwa na kitu fulani moyoni mwangu, ambacho ningependa kuzungumzia, labda kingekuwa m—msaada mkubwa kwenu, kufahamu sa—sababu ya kuhubiri Injili vile ambavyo nimejaribu kuhubiri Hiyo na kuiamini. Mnaona, ndiyo ile sababu Mungu amefanya. Siri za Injili zimefichwa tangu msingi wa ulimwengu, bali zilipaswa kufunuliwa katika siku hizi za mwisho. Basi kwa hiyo, Bwana akipenda, ninataka kuzungumza juu ya hilo.

19 Basi, kesho usiku ni ibada ya kufunga, nasi tungewatakeni mjitokeze ikiwa labda mngeweza.

20 Ndipo kutoka hapa kwenda Yuma, na kutoka Yuma kwenda Phoenix, na halafu kurudi. Tunaondoka kutoka huko, na halafu ninaondoka kwenda kwenye ziara fupi ya kuwinda, katika wakati wa likizo, likizo ya Krismasi, pamoja na baadhi ya rafiki zangu. Mke wangu anaenda kuwatembelea watu wake. Na—na halafu tunaenda kutoka pale, kufanya ziara kupitia California, na chini na juu magharibi, sehemu ya kusini ya Marekani hapa, kupitia Louisiana na Texas, na Florida. Ndipo basi kutoka huko,

nchi za ng'ambo, Bwana akipenda, kwa ajili ya utaratibu mrefu wa safari. Nami ninaomba maombi yenu.

21 Sasa, ni, ingekuwa sawa kama tungefurahia tu Uwepo wa nguvu Zake za uponyaji na kila kitu, bali kuna mengi yanayoambatana nayo zaidi ya hayo. Mnaona, mengi huambatana nayo. Halafu basi, hilo ndilo jambo, unapoanza kuingia ndani ya kitu, hiyo ni, hutatiza watu. Sasa, kila mtu aliamini katika uponyaji wa Kiungu, mbona, wangevutiwa tu moja kwa moja na huo uponyaji wa Kiungu, na kusema, "Asifiwe Mungu," na kupaza sauti na kuwa na wakati mzuri. Lakini basi nini kuhusu . . . Huo tu ni chambo kwenye ndoana, unaona, hiyo ni cha—chambo tu. Ndoana ndiyo hunasa samaki, nayo ndoana ni Neno. Sasa, Yesu alikuwa ni Mtu maarufu sana mradi tu Yeye aliwaombea tu wagonjwa.

22 Sasa, sisi si Yesu, bali ni—ni Yeye akifanya kazi kupitia sisi, sisi sote, pamoja. Yeye hayuko ndani ya mtu mmoja tu. Yuko ndani ya kila mwaminio. Hivyo ndivyo tunavyoamini kwa Uzima. Halafu basi, katika hilo, unaona, inaonyesha kwamba haijalishi ni kiasi gani Mungu angeweza kunitia upako, papa hapa kwenye mimbara hii, asipokutia upako kwa njia iyo hiyo, huko nje, hakuna kitu kitakachofanyika. Inahitaji sote wawili, pamoja. Sisi, inatubidi kuwa, sote wawili, kwamba hatuna budi sote wawili kuwa waaminio.

23 Isipokuwa kuwe na kitu ambacho Yeye anataka kuita, ili tu kuonyesha nguvu Zake kuu, mnajua, kuacha kitu fulani kifanywe kinachomfanya mtu fulani anayejaribu kufaya jambo lisilo sahihi, ama kitu fulani, Yeye angetaja hilo. Mnaona, bali inakubidi, tunaangalia tu hilo. Kwa kweli, wakati mwingine Yeye hutuambia mambo, na watu (taja) wanaambiwa mambo ambayo hawataki kusikia. Nami sitaki kulisema, bali, ikiwa Yeye ndiye anayezungumza, sisi tunasikiliza tu na kisha to—toba. Sasa wazia mambo haya, na uombe.

24 Pia kumbuka sasa, kama nilivyofananisha huduma Yake, unaona. Kwanza, nabii wa Galilaya, kila mtu alimwamini Yeye kuwa nabii. Lakini Yeye alikuwa "nabii," kuwaponya wagonjwa, bali wakati Yeye alipoanza kuingiliana na hao Mafarisayo na Masadukayo, na mapokeo yao, ndipo Yeye akawa "mwendawazimu." Wakasema, "Yeye ana kichaa." Hawakutaka uhusiano wowote na Yeye. Na hatimaye ikaletea kusulubiwa Kwake.

25 Na hivyo ndivyo ilivyofanya daima. Kote kupitia Bibliani, imefanya jambo lile lile. Na itabidi ifanye jambo lile lile huku, kwa kuwa ni Mungu. Itabidi ifikie mwisho huo hasa wa wakati. Bali kamwe hutasulubisha Ujumbe. Huenda ukamsulubisha mjumbe, bali kamwe hutasulubisha ujumbe wake kama umetoka kwa Mungu, maana ndio Ujumbe. Yeye ni mbebaji tu wa Ujumbe.

26 Sasa kwa kuwa tumekuwa tukizungumza kwa dakika chache, angalia, ni saa mbili kamili sasa, nami ninataka kufanya kanisa kuruhusiwa kuondoka saa tatu na nusu, kusudi mweze kupumzika na kufikia shule ya Jumapili. Basi kesho ni siku kuu. Hii itakuwa ibada mbili kwangu, leo. Na—na wakati nilipokuwa jamaa mdogo. . .Ibada mbili ni nzito kwa mhudumu yeyote, kama ukizichukua kwa moyo wako wote. Sasa ukienda tu hapo kwa mazungumzo mafupi ya kiakili, ungeweza kuzifanya kila dakika thelathini, arobaini, kote katika siku, na zisikusumbue. Bali kama ukiweka moyo wako wote hapo, ukishikilia Roho wa Mungu mbele za watu, hiyo ni tofauti.

Sasa hebu tuombe.

27 Baba wa Mbinguni, jalia baraka Zako na rehema zitulie juu yetu sasa, tunapoondokea mazungumzo yetu, kuingia kwenye Neno. Pia jalia Neno lifanyike mwili miongoni mwetu, tena usiku wa leo, ili kanisa kwa mara nyingine, sisi sote, pamoja, tuone, tuhisi, na kujua, Uwepo wa Yesu Kristo, Bwana wetu aliyefufuka. Kwa kuwa, tunampenda, Uwepo Wake ni Uzima kwetu. Basi jalia tupumzike, usiku wa leo, katika Utukufu wa Shekinah na kutambua kwamba ni Utukufu wa Shekinah, katika Uwepo Wake. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu, kwamba Yeye atatumegea Neno sasa. Amina.

28 Sasa geukeni katika Biblia zenu, kama mnapenda kufanya hivyo, kwenye Kitabu cha Marko Mtakatifu, mlango wa 4. Basi—basi fungu langu usiku wa leo, nitaliita, "Nenda kamwamshe Yesu." Basi somo langu usiku wa leo ni, *Kumwita Yesu Jukwaani*. "Nenda ukamwamshe," mwite jukwaani! Huu hapa usomaji wa Maandiko, kutoka katika Marko Mtakatifu, mlango wa 4, kuanzia kifungu cha 35.

> *Siku ile kulipokuwa* jioni*, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo.*
>
> *Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo.*

29 Hilo si lingefanya fungu la ajabu, "Mchukue Yeye jinsi alivyo"? Mchukue Yeye jinsi alivyowasilishwa kwako, unaona, mchukue katika chombo.

> *Na vyombo vingine vidogo vilikuwako pamoja naye.*
>
> *Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji.*
>
> *Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto; wakamwamsha, wakamwambia, Mwalimu, si kitu kwako kwamba tunaangamia?*
>
> *Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie. Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu.*
>
> *Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga? Imekuwaje hamna imani?*

Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, Ni nani huyu, basi, hata upepo *na bahari humtii?*

30 Nayo Maandiko yanasema, "Ni yeye yule!" Upepo na mawimbi humtii.

31 Hapana budi alikuwa amechoka kidogo siku hiyo. Mandhari yetu inampata Bwana wetu, usiku wa leo, tunapojaribu kuchukua kila wakati, mandhari ya mahali alipo, na kile Yeye anachofanya.

32 Ninapenda kumfuata, nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninapenda tu kumfuata Yeye na kuziona kazi Zake. Na kuwazia tu kwamba siku moja tutakuwa pamoja na Yeye na kumfuata Yeye, pamoja na Yeye, mwenyewe, kama vile kuona kwa hisi yetu ya kuona kama tunavyofanya sasa, na—na kuwa pamoja na Yeye milele. Loo, kumtazama tu Yeye, kungenitosha mimi. Kumwona tu Yeye, huko—huko—huko kungenitosha mimi.

33 Na sasa tunajaribu kuchukua onyesho, na tunamwona Yeye hapa mahali alipo, kile anachofanya. Halafu shida inainuka, na jinsi Yeye anavyoishughulikia shida hiyo, na kuwaambia ni kwa nini wasingeweza kufanya hivyo. Basi tunamkuta Yeye huko baharini, upande wa nyuma ya chombo. Alikuwa na siku nzuri sana. Hapana shaka ila kwamba mwili Wake ulichoka, na Yeye alikuwa ni mchovu. Na akijisikia amechoka na ni mnyonge, nguvu zilikuwa zimemtoka, kwa sababu alikuwa akihubiri na—na kuonyesha ishara Yake kuu kuwa Yeye alikuwa ni Nani, na kuwashuhudia watu, na kuwaponya watu.

34 Ndipo—ndipo umati, wengine walishangilia na wengine wakazomea. Hivi ungeweza kuwazia watu kumfanyia hivyo Yesu? Ilionekana kana kwamba wangeweza kujua vema zaidi ya hilo. "Vema," unasema, "kwamba . . . "

35 Wanafanya jambo lile lile leo hii, vile vile tu. Mnaona, kama akija leo hii, na katika jambo lilo hilo, jinsi alivyofanya wakati ule, watu leo hii "wangemzomea" Yeye na kumwita Yeye "mwendawazimu" kama tu walivofanya wakati ule. Mnaona, ingekuwa tu vile vile. Nao hufanya hivyo. Wasingeweza kumwelewa. Ulimwengu kamwe haukuelewa mwondoko wa kweli wa Mungu. Na kamwe hautatambua huo, kwa sababu ni ulimwengu.

36 "Ulimwengu haunioni tena," Alisema, "bali nyinyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, na nitakuwa ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu." Iwapo watu wangaliweza tu kuona nukuu hiyo moja kutoka Kwake, papo hapo, wangetambua mahali tulipo usiku wa leo.

37 Waweza kuwazia mtu ambaye hakuwahi kuwa na hisi ya kuona, hakuwahi kuona? Nawe ungejigonga kwa vitu. Ingekubidi kupata chakula chako kutoka kwa nishati, kutoka kwa bidhaa nyingine. Lakini unge—ungejigonga kwa kitu fulani.

Ulikuwa na hisi ya kugusa, bali si kuona. Ndipo basi, mara ghafla, mtu fulani aliyafungua macho yao, na kuona ulimwengu ulio tofauti kabisa. Hawakuwa wamewahi kuona chochote.

38 Na iwapo basi ungesema, "Vema, sasa, hilo linapaswa kuwa na joto kwelikweli ukilihisi, hilo ni jua."

"Jua ni nini?"

"Ni nuru."

39 "Nuru ni kitu gani?" Unaona, hakuwahi kuishi katika hisi hiyo. Hajui ni kitu gani.

"Kile ulichojigonga kwacho, ni kitu *fulani-fulani*."

40 "Vema, ni nini hicho?" Unaona, hajawahi kuishi katika awamu hiyo, hata kidogo. Kingekuwa ni kitu cha kigeni sana kwake, kukijua hicho.

41 Vema, sasa, Mungu akituacha tuishi, kimwili tupo hapa katika hisi tano. Bali kuna hisi nyingine. Halafu basi tukiamka katika hisi hiyo, na hiyo ni hisi ya ono, na tunaona kitu hicho, kwamba ni kitu gani ambacho hutufanya kuhisi vitu hivi tunavyohisi. Na kujaribu kumwambia mtu mwingine kuhusu Hilo, itakuwa tu kama kumwambia mtu ambaye hakuwahi kuona, katika maisha yake. Asingeweza kuelewa hilo, kwa sababu ha—hana mazoea ya hisi hiyo. Na hivyo ndivyo ilivyo katika Injili. Wao, wao hawaielewi. Ni vigumu kuwafanya waione, kwa sababu kwamba hawajawahi kuishi humo ndani. Hawajui chochote kuihusu. Wanaihisi, na wao—wao wanaweza kuiitikia; bali kujua kweli kwamba ni nini, hatujui. Kwa hiyo basi wakati unapoweza kuona kupita lile pazia, mahali hilo hutoka, na kisha ujaribu kurudi na kuwaambia watu ambao wamelihisi tu kwa hisi ya kugusa, kwa mfano, na kamwe hawajawahi kuliona, ni vigumu kumwelezea mtu. Lakini inakubidi tu kufanya kadri uwezavyo mpaka "sote tuone uso kwa uso."

42 Sasa tunamwona Yesu hapa, amechoka, ni mchovu, nami ningewazia tu, Yeye akijua kuna kazi kubwa kesho yake, mbele Yake, huko Gadara, ambapo palikuwa na nafsi moja iliyokuwa ikimwitia Mungu. Je! waweza kuwazia Yesu akichukua. . . amechoka na ni mchovu, na anavuka bahari yenye tufani, ili kuifikia tu nafsi moja? Lakini Yeye hufanya hivyo. Hivyo ndivyo Yeye hufanya.

43 Chombo kilikuwa kinavuka, ndipo Yeye akachukua fursa hii kupumzika kidogo, kuamka. Basi wanafunzi Wake walikuwa wamerudi kwenye makasia yao na kazi zao za kila siku, kile walichofanya. Uamsho wa siku hiyo ulikuwa umeisha.

Kitu kama leo hii, naamini. Naamini ni kitu kile kile.

44 Na kwenye wakati huu, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa amechukua pumziko kidogo, labda kati ya mikutano tu. Ndipo wanafunzi wakarudi kwenye shughuli zao za kale.

45 Sasa hebu tupenye tu tuingie kwao, ninaamini huenda walikuwa wakishangilia, wakizungumza juu ya mambo waliyokuwa wameona yakifanywa siku hiyo. Kulikuwako na mambo makuu yaliyotendeka. Watu walikuwa wameponywa, ukoma. Nao walikuwa na wakati mkuu. Basi walipoendelea na kazi yao kanisani, ama wao. . . Kanisa si jengo; ni watu wanaolifanya kanisa. Basi walikuwa wakishangilia katika kile walichokuwa wameona kikifanywa. Na huenda walikuwa wakijadili umasihi Wake, madai Yake; Yeye alidai kuwa ni Neno, alidai kuwa Neno na ujumbe wa wakati huo.

46 Naye nabii, ambaye alikuwa Neno kabla ya hapo, alimtambulisha, na kasema, "Wakati wangu umeisha. Nimetimiza sehemu yangu, Neno nililopaswa kutimiza. Sasa Yeye anaenda kudhihirisha Neno lililosalia, kuanzia hapa kuendelea, kwa hiyo wakati wangu umekwisha," Yohana, kwa hiyo ilimbidi kuondoka jukwaani wakati Yesu alipokuja jukwaani.

47 Ndipo wakati Yeye alipokuja jukwaani, Yeye alikuja hasa, na kufanya hasa, na kutenda hasa kabisa jinsi Masihi alivyopaswa kutenda, yale aliyopaswa kufanya. Na hayo huenda yalikuwa ndiyo majadiliano yao walipozungumza.

48 Labda baadhi yao walikuwa na ushuhuda. Mmoja wao angesema, "Mnajua, sikuwa nimefikiria ku—kuhusu hilo sana mpaka nilipoanza kusoma Maandiko kile Masihi alichopaswa kuwa, kwa sababu Yeye alikuwa awe yule nabii. Na halafu ninasikia ya kwamba, jambo jingine, nilipomwona akiumega ule mkate na kuwalisha wale watu. Ni nani aliyeweza kuumba, ila Mungu Mwenyewe? Kwa hiyo huyo hana budi kuwa ni Masihi." Na, wao, "Hakuna mtu awezaye kuumba ila Mungu. Mungu ndiye Muumba pekee aliyepo. Basi hapa Yeye alichukua biskuti tano ndogo ndogo na samaki wawili wadogo, na kulisha watu elfu tano, na kuokota vikapu saba vilivyojaa, vipande vilivyobakia. Wakati, hakuna kitu kilichoweza kufanya hivyo ila Yehova, Yeye yule aliyenyesha mkate kutoka angani. Huyo Ndiye pekee aliyeweza kufanya hilo. Naye Huyu hapa, anayejulikana miongoni mwetu, katika umbo la seremala mnyenyekevu, Mtu wa kawaida. Huyu hapa Yehova aliyeishi Mbinguni, hakuna aliyeweza kumwona Yeye; Mungu asiyeonekana amefanywa aonekane hapa miongoni mwetu, kwa kuwa, tunamjua Yeye, Yeye hufanya kazi zile zile Yehova alizofanya."

49 Basi Yeye aliwaambia, "Ikiwa sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Masihi alipaswa kuwa ni Yehova, *Imanueli*, 'Mungu pamoja nasi.' Basi nisipozifanya kazi za Imanueli, nisipotenda kama huyo Imanueli, kazi Zangu si kama za huyo Imanueli, basi—basi mimi si Imanueli. Lakini ikiwa hamwezi kuniamini Mimi, angalieni tu kazi nizifanyazo. Zinanishuhudia kuwa mimi ni Nani." Mnaona?

50 Na hayo huenda yalikuwa ni majadiliano yao walipokuwa wakizungumza. Ndipo basi mada hiyo huenda ilitokea baada ya hapo, wakati . . . Labda wengi wao wangekuwa wameshuhudia. Kulikuwako na Andrea, huenda alishuhudia.

51 Petro huenda alisema kile Yesu alichomwambia. "Mbona, kuniita kwa jina langu? Ni nani angeweza kujua jina langu ila Mungu? Aliniita lile lililokuwa jina langu. Aliniambia kuwa mimi ni nani. Akataja jina la baba yangu, na Mtu huyo kamwe hakuwa ameniona. Mbona, haina budi kuwa ni Masihi. Nasi tulitambua."

52 Sasa tunaona, basi, kwamba huenda walijadili mitazamo ya watu kuhusu Hilo. Hayo huenda yalikuwa ndiyo majadiliano yao yaliyofuata. Yesu alikuwa analala muda wote; alienda nyuma kupumzika. Sasa hebu tupenye tu tuingie jukwaani na kuwatazama; mitazamo ya watu. Baadhi yao walisema . . .

53 Vema, baadhi yao waliamini. Baadhi yao wakasema, "Hakuna mtu aliyewahi kunena namna hii hapo kabla. Kwani, yale asemayo Mtu huyo, Mungu huunga mkono yale asemayo. Nasi tunajua, kwa Maandiko ye—yetu, kwamba ikiwa Mungu anamthibitisha Mtu huyu, yale Yeye asemayo yanatimia, basi tunajua kwamba Mungu yu pamoja na Mtu huyo. Naye Mungu ametwambia kumwogopa Mtu huyo, kwa sababu Yeye yuko pamoja Naye. Neno Lake ni Neno la Mungu, kwa hiyo mwogopeni Yeye." Ndipo wao—wao wakasema . . . Sasa, hiyo ndiyo sababu waliogopa sana baada ya kumwona akitiisha upepo na mawimbi. Walitetemeka kwa sababu walijua huyo alikuwa ni Mungu. Ilibidi kuwa hivyo. Mungu aliliheshimu Neno Lake. Kile alichosema, kilitukia, ndipo wakajua huyo alikuwa ni Masihi.

54 Sasa, walipokuwa wakijadili mitazamo, walisema, "Baadhi yao waliamini, na wengine wasingeweza kuamini."

55 Sasa, daima tunapata hilo miongoni mwa makanisa, kila kusanyiko, tunakuta matabaka matatu ya watu. Kusema kweli, nilihubiri juu yake, hapa si muda mrefu uliopita, ninaamini kwenye Mji wa New York, ama mahali pengine, juu ya matabaka matatu ya watu. Na, hayo ni, waaminio, wasioamini, na wanaojifanya waaminio. Na sura moja tu ama mbili baada ya hapa, tunakuta kwamba watu Wake Mwenyewe walifikia hilo, na kuthibitisha hasa kwamba hivyo ndivyo walivyokuwa. Sasa hebu tuwazie tu kuhusu waaminio na wasioamini, kwa sekunde tu hapa.

56 Waaminio ndio wale waliokusudiwa na kuchaguliwa kwa Neno. Dakika ile wanapoliona Hilo, wanaridhika, Uhai huchipuka ndani yao na wanakubali Hilo. Hao ni wanafunzi. Hamna swali niani mwao kuhusu Hilo, hata kidogo. Wanafuata moja kwa moja. Wanafunzi walikuwa ni waaminio. Waliamini.

57 Sasa, mara nyingi, asiyeamini halisi atajifanya kwamba anaamini. Sasa, asiyeamini alikuwa ni kama wale sabini, walifuata moja kwa moja katika umaarufu na mambo ya kuvutia ya huduma Yake. Walifurahia kusimama pale wakati Yeye alipowafufua wafu na kutakasa wenye ukoma, na—na kutabiri mambo yaliyokuwa yakitimia sawa hasa. Lakini siku moja Yeye alinena jambo fulani, nje ya kanuni zao za imani. Na punde tu Yeye aliposema jambo lililohitilafiana na kile walichoamini, wale sabini wakasema, "Hili ni jambo gumu, kasema, 'Mtasema nini mtakapomwona Mwana wa Adamu akishuka juu Mbinguni mahali alikotoka?' Sasa, Mtu huyu tunayelala pamoja naye, Mtu huyu ambaye hula pamoja nasi, Mtu huyu ambaye hunawa uso wake na mikono katika beseni ile ile tunayonawia, Mtu huyu ambaye hula kama mimi, hulala kama mimi, aliye na heri na shari Zake, na kusema ati Yeye alishuka kutoka Mbinguni? Hayo yamenizidia mimi." Unaona? Basi walifanya nini? Wasingeweza kukaa mpaka mwisho wa mkutano. Walisimama na kuondoka. A-ha. Unaona? Yaliwatosha. Hao ni wasioamini. Unaona? Wasingevumilia hayo. La, bwana. Waliondoka na hawakutembea na Yeye tena.

58 Sasa, kuna waaminio ambao...hakuna kitu kiwezacho kuwatenga na Hilo.

59 Halafu kuna wasioamini, na punde tu chochote kinaposemwa ambacho hakikubaliani na kile wanachoamini. Kumbukeni, Biblia inatufundisha kwamba asiyeamini atakuwa karibu sana kama mwaminio halisi, hata itamdanganya Mteule kama yamkini. Mnaona, huko ni kutokuamini. Lakini punde tu jambo fulani linaposemwa ambalo hawalipendi, kwisha. Mnaona, huko ni kutokuamini. Hiyo inaonyesha kabisa.

60 Wakati Nuru ya Uzima inapoangaza, kuileta mbegu hiyo, Hiyo ingefanya nini juu ya jiwe? Haitafanya chochote. Ingefanya nini juu ya kitu kilichokufa? Haijatumwa kwa vitu vilivyokufa. Jua huwaka kwa ajili ya mbegu iliyorutubishwa kwa uhai. Nayo Biblia hii na Neno Lake, katika saa tunayoishi, inawaangazia hao kushika Uzima wa Milele, wale waliokusudiwa kuona Hilo. Na halitafanya chochote chema juu ya hao wengine. Hamna uhai mle kuchipuzwa na jua, ama na Nuru.

61 Basi tunaona, kwamba waligeuza migongo yao na kuondoka na hawakutembea na Yeye tena. Hapo ndipo jambo kuu lenye fahari lilisemwa kuhusu... Simoni Petro alisema. Yesu, baada ya wale sabini kumwacha Yeye, wakati aliposema, "Vema, nini..." Aliwapa Fundisho fulani gumu. Yeye, siku Zake za uponyaji zilikuwa karibu zimekwisha. Hakujali, hakuwa anaenda kuwaponya wengine wengi zaidi. Alikuwa anaenda kuwaambia kuhusu kitu fulani kilichokuwa bora. Ndipo Yeye akasema, alianza kuwaambia hayo, Yeye hapo aliwafunulia Yule hasa Yeye alikuwa. "Mtasema nini mtakapomwona Mwana wa Adamu akishu-...akipaa juu Mbinguni kule alikotoka?"

62 "Sasa tuna rekodi Yako ya kuzaliwa hapa. Ulizaliwa na Mariamu na Yusufu, huko chini Nazareti. Na hapa Wewe unasema ulishuka kutoka Mbinguni? Vema, hiyo ni . . . Wewe, Wewe una wazimu, ninaamini. Mnaona? Vema, tusingetaka kumfuata Mtu kama huyo." Kwa hiyo, wakaondoka. Wakaenda. Hao ni wasioamini.

63 Lakini angalia sasa, kunao waaminio. Haijalishi kinachofanyika, kinachotendeka, jinsi ilivyo vigumu, jinsi ilivyo ya ajabu, wanaamini, hata hivyo. Hiyo ni kama mwanamume ama mwanamke aliyeombewa. Wanaamini hilo. Hakuna kitu kinachoenda kuwafanya wabadili nia yao. Hao ni waaminio halisi. Na hakuna kitu, haijalishi inavyoonekana kuwa ngumu, kile *hiki* kilicho, na *hiki* hakitendeki, hiyo haina uhusiano na Hilo. Wao wanaamini Hilo, kwa vyovyote vile.

64 Sasa, huenda alisema mambo mengi ambayo wanafunzi hawakuamini, ama hawakuona, bali waliamini Hilo, kwa vyovyote vile. Waliendelea moja kwa moja na Hilo, kwa sababu walikuwa na hakika Maandiko yalikuwa yamemtambulisha Yesu kabisa kuwa ni yule Masihi.

65 Nami ninaamini Maandiko leo hii yanatambulisha kabisa huduma hii kuu ya Mungu katika siku za mwisho, ya Roho Mtakatifu, kuwa ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninaamini Maandiko kabisa yanatambulisha Hilo. Sijali yale mtu yeyote mwingine anayofikiria kuhusu Hilo, tunaamini Hilo kuwa ndilo Kweli kwa sababu limetambulishwa kikamilifu.

66 Unasema, "Ndugu Branham, ninajua unaelewa Hilo." Silielewi. Ninaliamini tu. Siwezi kuelewa mambo haya. Sijaribu kuelewa. Huwezi kumwelewa Mungu, Yeye hana budi kukubalika kwa imani. Nayo imani ni kitu ambacho unaamini, ambacho huwezi kuelezea. Haya basi. Hiyo hapo Kweli.

67 Sasa, kuna kundi jingine ambalo daima hushikilia karibu, na huyo ni mwaminio wa kujifanya. Sasa, huyo mwaminio wa kujifanya anachukuliwa kuwa ni mnafiki.

68 Sasa hebu tumchukue anayejifanya mwaminio. Ilikuwa ni Yudasi. Alikuwa ni mwaminio wa kujifanya. Naye mwaminio wa kujifanya hushikilia na kushikilia, akijaribu kupata njia fulani ya kuwawezesha kupata kitu fulani juu ya Hilo. Wanashikilia karibu kwa muda mrefu kutosha ili tu kuona ikiwa hawawezi kupata kasoro kidogo, halafu waondoke na kuifichua mahali fulani. "Tunataka kuona ni ujanja wa aina gani, ni mguu gani wa sungura ulio nao uliosuguliwa nyuma ya masikio yako. Ni nini ujanja?" ili waweze kuiga Hilo, ama kitu fulani. Hao ni waaminio wa kujifanya. Hao ni wa Yudasi.

69 Hao ni wasioamini, waaminio wa kujifanya, na waaminio. Hao watatu wangalipo kila mahali kote ulimwenguni. Daima wamekuwa nao, na daima watakuwapo. Sasa wazia hilo usiku

wa leo, hapa na kwenye kanda hii kwa wale watakaosikiliza. Haya matabaka matatu yanayoketi, ni matabaka matatu ya watu hao daima wanaokutanika.

70 Moja, hilo halileti tofauti kile kinachotendeka, wangali wanaamini Hilo. Wameshawishika kabisa.

71 Wengine wataamini kiasi fulani cha Hilo, na halafu hawataki kuamini hayo mengine. Hao ni wasioamini.

72 Halafu basi waaminio wa kujifanya ni wale wanaoshikilia, watashikilia tu karibu mpaka wanapoweza kupata kitu fulani. Wanasema, "A-ha, haya basi. Jambo ndilo hilo. A-ha, hapo, nilidhania kulikuwa na kitu. Haya basi!"

73 Bali mwaminio halisi, hayo hayamyumbishi hata kidogo. Hakuna kitu kinachomyumbisha.

74 Vipi kuhusu Yesu akisimama pale, mate usoni Mwake, na damu usoni Mwake, na taji ya miiba juu Yake, na—na yote Yeye aliyokuwa nayo pale, kundi la kudhihaki, na kadhalika? Vema, asiyeamini angewazia nini kuhusu hayo, ama mwaminio wa kujifanya? Walimsaliti tu. Ndipo, unakuta kwamba, mwaminio wa kujifanya ndiye anayekusaliti. Huyo ndiye anayeharibu huduma yako, ni huyo mwaminio wa kujifanya.

75 Bali mwaminio halisi, haijalishi ni nini, wameridhika kabisa. Wameshawishika kabisa, kwa sababu Uhai uliomo ndani yao tayari umefanyika Kristo. Ni Kristo. Si wewe tena, bali ni Kristo anayeishi ndani yako. Basi, haijalishi, "Hakuna kitu," Paulo alisema, "kilichopo, kitakachokuwapo, mauti, hatari, uchi, chochote kile, kiwezacho kututenga na upendo huo wa Mungu ulio katika Kristo." Hapana, mengi, ni idadi gani ya *hiki*, *kile*, au *kinginecho*, kuinuka, ni Madaktari wangapi wa Uungu wanaoweza kujaribu kueleza Hilo vinginevyo na kusema Hilo ni kwa ajili ya siku nyingine, hayo hayakutenganishi hata kidogo. Upo hapo kudumu. Ni wewe ndani ya Kristo, wewe si wako tena. Huyo ni wewe, wewe na Mungu, pekee.

76 Na punde tu asiyeamini anapoweza kupata mwanya, anajaribu kuondoka hata hivyo, kwa hiyo anaondoka.

77 Mwaminio wa kujifanya anakaa muda mrefu kidogo, mpaka anapoweza kupata kitu ambacho anaweza kuwekea pingamizi juu Yake.

78 Kwa hiyo hao hapo watatu wako, wote pamoja. Hao ndio aina waliokuwa nao wakati ule. Hao ndio aina walio nao sasa. Hao ndio aina watakaokuwa nao mpaka Yesu Mwenyewe, ama Mungu kwenye Hukumu Kuu ya Kiti Cheupe Cha Enzi, atawatenganisha.

79 Wengine walisema, "Hakuna mtu aliyewahi kunena kama Mtu huyu. Yale asemayo hutimia."

80 Wengine, wasioamini, walisema, "Yeye ni Beelzebuli. Yeye amerukwa na akili. Mtu huyo amerukwa na akili."

81 Mnajua, kuna jambo kubwa ambalo Shetani hujaribu kufanya. Yeye hujaribu kufanya m—m—mjumbe, watu ambao wamepokea Roho Mtakatifu, wajaribu kusema kwamba, "Wamerukwa na akili."

82 Nilipata barua ndogo ya matangazo, barua juu ya hilo hivi majuzi, huko nje, kasema, "Maskini Ndugu Branham!" Kasema, "Tuliamini kwamba yeye alikuwa ni Eliya." Pia kasema, "Mnajua kwamba—kwamba, mnajua, alirukwa na akili." Tena kasema, "Vazi la Eliya lilimwangukia Elisha, huyo alikuwa ni mke wangu. Basi yeye anachukua huduma, kuendelea na sehemu maradufu." Mwanamke? Hivi ilikuwa, hivi Eliya alipoteza akili yake, ama alitwaliwa juu pasipo mauti, katika gari, kwenda Mbinguni? Hum! Mnaona? Lakini, unakuwa tu na hilo, unaona, hilo—hilo ndilo linalotubidi kukabiliana nalo.

83 Baadhi yao walisema, asiyeamini, kasema, "Jamaa huyu ni Beelzebuli."

84 Hapana budi ilikuwa ni Yohana, kasema, "Wazia tu juu ya Huyu Ambaye hufanya haya yote!" Sasa imerudi kwa waaminio tena. Kasema, "Wazia tu, Yule ambaye—ambaye amefanya haya yote ambayo tunawazia na kuzungumzia, na matamshi ya watu mbalimbali! Sisi sote ni waaminio," akasema. "Tunaamini Hilo. Naam, bwana. Tumeridhika kwamba tunajua kuwa kwa kweli limetambulishwa. Ndiye Yule pale amelala, Mtu apatikanaye na mauti, amelala pale moja kwa moja kwenye sitaha, pale pale nyuma katika kitu kama, chumba kidogo cha kulala, amelala juu ya mto. Tulimweka huko nyuma, amelala. Lakini wazia hilo! Mungu mwenyewe wa maumbile anasafiri kupitia maji haya pamoja nasi." Loo, jamani! Amina.

85 Hayo maji yalikuwa hatari. Mnajua, dhoruba ilitokea na ingali inafanya jambo lile lile, ikiwa uko karibu na Yerusalemu. Nadhani, Jack, unakumbuka. Dhoruba hizo zingali zanafagia moja kwa moja kupitia ule ufa pale, na kuigonga hiyo bahari na kuzamisha wavuvi, kama tu ilivyofanya wakati ule. Inakuja, hata huwezi kuona dhoruba ikija; mara moja, iko hapo.

86 "Basi wazia tu sasa, sisi sote, maisha yetu yote, tumeogopa kuyavuka maji haya hatari hapa. Lakini kumbukeni, Yule hasa tunayemjua kuwa ndiye Muumba, amelala pale pale ndani ya chombo, pamoja nasi. Najisikia vema! Na nyinyi je, wavulana?" Wangesema, "Amina. Naam, bwana. Ndiye Yule pale ndani ya chombo!"

87 Na jinsi lilivyo muhimu kuijua siku tunayoishi, kwamba walikuwa wameona utambulisho, kwamba, na waliridhika, haijalishi kile mtu yeyote mwingine alichosema. Mazungumzo yao yalikuwa yanahusu waaminio, na wanaojifanya waaminio, na kadhalika. Bali wao wenyewe waliamini Hilo. Na walijua kwamba walikuwa na Yeye pamoja nao. Haijalishi kile yeyote wa watu hao wengine, walikuwa na furaha kuwa na Yeye.

88 Nami, pia. Na nyinyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Haijalishi kile ulimwengu wote usemacho. Nina furaha kujua kwamba Yeye anasafiri bahari za maisha yenye tufani pamoja nami, moja kwa moja chomboni. Amina. Amina. Kusafiri kupitia bahari zenye heshima, kama Yeye afanyavyo, na katika maji yote yenye hatari, bila kujua ni wakati gani ungeweza kupigwa risasi, kuuawa, uanguke umekufa, chochote kinachoweza kutukia. Bali Muumba . . .

89 Wewe ni kitu gani, hata hivyo? Wewe ni bonge dogo la udongo wa Louisiana, lenye uhai fulani ndani yake. Hayo tu. Hata kama unatoka Texas, mahali pale pakubwa, wewe ungali tu ni bonge la matope ya Texas lenye unyevu kidogo ndani yake. Na hayo tu ndiyo uliyo. Hiyo ni kweli kabisa. Na hayo ndiyo unayorudia.

90 Lakini, hata hivyo, matope hayo yangewezaje kutembea, kupumua, kula, kama hakukuwa na uhai fulani ndani yake? Pia, wazia, yalibidi kuumbwa! Na Muumba mwenyewe aliyeyaumba, anasafiri ndani ya chombo hicho cha udongo. Amina. Alinifanya kile nilicho, bila ombi; ni zaidi sana jinsi gani Yeye anavyoweza kunifufua kwa shauku yangu, kwa Neno la ahadi Yake!

Kusafiri juu ya bahari adhimu ya maisha,
Tunapaswa kuishi kama Yeye, tuache Roho
  Wake, afanye kazi kupitia sisi;
Kwa ajili ya ndugu mpweke na aliyetupwa na
  meli baharini,
Katika kuona, atajipa moyo tena.

91 Wazia, Yeye yu pamoja nasi, kwa usalama. Ni hisi ya jinsi gani ya usalama, wakati tunaposafiri maji haya yenye hatari! Hapana shaka ilikuwa kitu kama sisi sasa hivi kwenye wakati huu wa sasa, baada ya uamsho, tukiyafurahia matokeo.

92 Ninaikumbuka safari yangu ya kwanza kwenda Shreveport, Louisiana. Sikuwahi kusikia kuhusu Jack Moore, na ninaamini ilikuwa ni Ndugu Richard Reed (sijamwona Ndugu Reed kwa miaka) ambaye aliniambia kuhusu Ndugu Moore hapa chini, ama Ndugu Kidson; mmoja wa ndugu hao, ninasahau ilikuwa ni nani sasa. Nilimzoea Ndugu Jack. Nikaja hapa chini. Maskini mpendwa mama yake mkongwe, ameketi karibu hapa mahali fulani. Naye alikuwa na ugonjwa wa tumbo, basi tukamwombea. Alikuwa anakula chakula cha mtoto. Ameweza kula tangu wakati huo, kawaida yake, chakula chake cha kawaida. Na jinsi—jinsi, ni uamsho mkubwa jinsi gani ulioinuka, uliongoza ndipo moja kwa moja wakaja Billy Graham na Oral Roberts, na—na Tommy Osborn, watu mashuhuri, mashujaa, walikuja kutoka kwenye maskini . . . wakatokea upesi kutoka kwenye uamsho, wakafanya mambo makubwa.

93 Siku hiyo kule chini, yapata miaka thelathini na mitatu iliyopita, ama thelathini na nne, nikisimama kwenye kingo za Mto Ohio kule, kwenye daraja, na yapata watu elfu tano

au zaidi walikusanyika kwenye kingo. Nilikuwa na yapata umri wa miaka ishirini, ishirini na tatu, ishirini na mbili au umri wa miaka ishirini na tatu, uamsho wangu wa kwanza. Nilikuwa nikibatiza watu mia tano, alasiri hiyo. Nao mashemasi walikuwa wameniongoza kuingia majini. Yapata mtu wa kumi na saba, nilipokuwa nikibatiza, nilisikia Sauti ikisema, "Tazama juu." Ndipo nikageuka kutazama juu. Mama yake Billy, hata hatukuwa tumeoana wakati huo, tukichumbiana tu. Hii hapa ikaja ile Nguzo ya Moto, ikizunguka katika anga angavu za bluu, kwenye saa nane tarehe 15 Juni, ikija moja kwa moja chini kutoka angani, namna hiyo. Ndipo Sauti ikanguruma, kote mahali pale, na kusema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, unao Ujumbe ambao sasa utatangulia Kuja kwa pili kwa Kristo." Wapiga picha wakipiga picha.

94 Tungewezaje kuamini hayo, na elimu haba ya shule ya msingi, na kadhalika? Lakini niliamini. Alasiri hiyo, nilipokuwa nimechoka sana nilipomaliza kubatiza, iliwabidi kuja kunitoa majini. Nisingeweza kuvumilia zaidi mkondo wa mto.

95 Basi Hiyo ikaenda, ikashuka, nao wakapiga picha Zake. Ilikuwa kwenye Associated Press, ikaenea karibu kote ulimwenguni, ikaingia huko Canada. Ndugu Lee Vayle angali ana nakala yake, nadhani, kutoka kwenye Associated Press, "Nuru ya ajabu yaning'inia juu ya mhudumu wa kawaida wa Kibaptisti wakati akibatiza chini ya Barabara ya Spring huko Jeffersonville, Indiana." Louisville Herald iliiandika, ikapiga picha, na ikatangaza, na ikaenda kwenye Associated Press.

96 Sasa, hiyo imekuwa ni miaka mingi iliyopita. Ingewezaje kuwa hivyo? Bali ilikuwa hivyo. Mungu alisema hivyo, hiyo inaifanya kuwa sahihi. Na ni ki—kitu chenye utukufu jinsi gani kujua kwamba tunaye Mungu aishiye! Ndipo kutoka hapo akaleta mioto ya uamsho kote ulimwenguni. Na sasa mikutano mikubwa ya uponyaji na mambo makubwa ya ajabu yemeendelea.

97 Wakati nilipokuja miongoni mwenu mara ya kwanza, nilisema ingenibidi kukushika mkono, na kukushika tu namna hiyo kwa ajili ya kiunganisho. Ndipo basi nisingewazia kile nilichokuwa ninaenda kusema, nawe ungeona matokeo yake. Bado hufanyika, na kuiona namna hiyo.

98 Ndipo basi akaniambia, "Kama utakuwa mwaminifu, itatimia kwamba utajua siri hasa ya moyo wao." Nyinyi nyote, wengi wenu enyi watu mnakumbuka hilo. Na ikaja kutimia, namna hiyo tu, sawa kabisa. Miaka michache baada ya hapo, nilikuwa huko juu katika Jiji la Malkia, Regina, Canada, na nikisimama jukwaani, pamoja na Daktari Ern Baxter na wengine. Ndipo mtu akaja akitembea kupitia jukwaani. Na jambo la kwanza, hata sikujua nilichokuwa nikisema, nikaita

jina lake, nikamwambia kilichokuwa shida yake, na hapo ikatukia. Tangu hapo, ikaendelea.

99 Sasa imefikia kiwango kingine. Kwamba siwezi kujua, bali itanena yenyewe.

100 Lakini kumbuka, katika huduma kuu, ilianzisha moto wa uamsho na kuenda kote ulimwenguni. Na sasa, katika miaka michache iliyopita, uamsho huo ulidumu muda mrefu kuliko uamsho wowote tuliopata kujua katika historia. Hakuna mwanahistoria awezaye kusema kwamba uamsho ulidumu kwa nadra zaidi ya miaka mitatu, kwenye wakati wowote. Bali huu umeendelea miaka kumi na mitano, au zaidi, uamsho wa moja kwa moja usiobadilika.

101 Lakini sasa uamsho umefifia. Ni nadra sana. . . Ndipo kukaja Mvua ya Vuli, na mkia wake mdogo kwa namna fulani unafagia kupitia Uingereza sasa, na huko nguvu zake za mwisho karibu zimeisha. Kanisa limetulia katika Laodikia tena, kufanya wakati. Inabidi iwe hivyo. Hasa, lazima iwe hivyo. Na sasa tunasherehekea usiku wa leo juu ya ma—makombo ambayo tunaokota kutoka kwenye uamsho huo.

102 Hiyo karibu ni kama wale wanafunzi walivyokuwa kutoka kwenye uamsho wa siku hiyo, wakingojea siku iliyofuata. Yesu, kwenye wakati huo, alikuwa akipumzika. Labda Yeye alikuwa akipumzika kutoka kwa uamsho huo, kama vile Yeye alivyokuwa akipumzika kwenye siku ya saba; baada ya kuumba dunia katika sita, ndipo Biblia ikasema, "Alipumzika. Alipumzika, siku ya saba." Vema, labda hiyo ndiyo Yeye aliyokuwa akifanya. Alikuwa akipumzika.

103 Ndipo, ghafla, shida ikaingia. Loo, acha Kanisa lianze tu kupumzika kidogo, na ndipo shida inaingia. Chombo kikaanza kuyumba, matanga yakaenda na upepo, nayo maji yakajaza chombo. Ilionekana kana kwamba matumaini ya kunusurika yalikwisha. Ingawa walikuwa wamemwona Yeye akifanya mambo mengi sana, shida inapoingia . . .

104 Sasa hapa ninaenda kufunga katika dakika chache tu, maana tunaenda kuanzisha mstari wa maombi.

105 Tumeona mambo hayo yote. Tumeona uzuri na ubaya wa watu. Na sasa inafikia mahali ambapo kwa namna fulani imelegea, tunazungumza kuhusu yale ambayo Yeye amefanya, na kadhalika, na kutazamia yale ambayo Yeye anaenda kufanya. Huo ni ubinadamu tu. Wanadamu daima wanazungumzia yale ambayo Mungu alifanya, yale ambayo wanaamini anaenda Kufanya, na kusahau yale ambayo anafanya.

106 Walifanya jambo lilo hilo. Walikuwa wamemwona huko nje akiwaponya wagonjwa na kufufua wafu, na kujua mambo kimbele, na kuwaambia watu siri za mioyo yao, na kuamini kwamba walikuwa njiani kuelekea uamsho mwingine. Lakini shida ilipoingia, walisahau yote kuhusu hayo.

107 Hivyo ndivyo tufanyavyo. Hapo ndipo tunapoketi usiku wa leo, tumeketi mahali papo hapo. Na hata hivyo, kama tu tungalijua, Yeye yumo chomboni. Yeye ni mkuu tu hapa sawa na alivyokuwa wakati alipokuwa amelala katika kile chombo. Yeye ni mkuu tu kama alivyokuwa wakati aliposimama katika utupu na kuumba ulimwengu. Yeye ni mkuu tu sawa na alivyokuwa pamoja na Musa, kwenye Bahari ya Shamu. Yeye ni mkuu tu kama alivyokuwa kwenye kaburi la Lazaro. Yeye ni mkuu tu kama alivyokuwa wakati Yeye alipomponya mwenye ukoma, akamfungua macho kipofu. Yeye ni mkuu kama alivyokuwa katika siku za uamsho wa Welsh. Yeye ni mkuu tu kama alivyokuwa katika wakati wowote, na Yeye yupo hapa ndani ya chombo!

108 Shida iliingia. Tunaenda mahali mbalimbali, tunakuta mizozo kanisani, utengano. Je! unajua hayo yataharibu kanisa? Dumuni pamoja!

Kibarikiwe kifungo kifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa nia ya udugu
Ni kama wa ule huko juu. (Upendo huo uwezao kushirikishwa na imani kwa Mungu na mmoja kwa mwenzake!)

109 Lakini tunaona sasa, ugavi wa maji unapunguka. Na katika nchi yangu mahali ninakoishi huko Tucson, kila kitu huko nje kina mwiba juu yake. Kila—kila kitu unachoona kina mwiba, na kwa sababu ni kukavu sana. Sasa, kama kingekuwa hapa katika nchi hii, na kingekua, kingekuwa na jani jororo kabisa. Mwiba huo ni jani lililokunjamana, ni gumu sana na lenye ncha kali, hakuna kifaa kinachoweza kunolewa kiwe kama huo. Hakuna kifaa kinachoweza kunolewa kuwa kama dungusi, maana una kidevu juu yake, kulabu ndogo, kote kuteremka mpaka chini. Na bado usingeweza kunoa kifaa namna hiyo, bali maumbile yameukunja, huo. Na utaruka moja kwa moja juu yako. Haikulazimu ku—kuingia katika huo; unakushika.

110 Na hivyo ndivyo ilivyo na dhambi. Haikubidi kuingia ndani yake; inakuja juu yako. Itakurukia. Usiikaribie. Kaa mbali na kutokuamini! Lakini tunaishi kwenye wakati huo.

111 Kwa hiyo walikuwa wamemwona Yeye akifanya mambo mengi sana makuu, nao wangeweza kuzungumza juu yake. Lakini wakati wa shida ulipowadia, yote yalisahaulika.

112 Sasa wazia tu mambo ambayo tumemwona Yeye akifanya, pamoja na thibitisho lisilokosea la utambulisho wa Neno Lake, na kujua kwamba ninii—kwamba Roho Mtakatifu mkuu hapa katika siku za mwisho ndiye Mjumbe wa wakati huu. Yeye ndiye Yule Ambaye anatuthibitishia, na kufanya kila ahadi ambayo Yeye aliahidi kufanya, kila ishara na kila kazi, na kila Neno kutimia jinsi tu Yeye alivyosema kwamba atafanya.

113 Na ingali inadharauliwa. Kama lingalikubalika katika madaraja makubwa ya juu, ningaliliondokea. Lisingeweza kuwa ni Mungu na likubalike huko juu. La, bwana. La, hasha, kamwe haitakuwa, kama lilikubalika. Lakini kwa sababu Hilo liko chini *huku*, hiyo ndiyo sababu ninaamini Hilo. Mnaona? Hapo ndipo linapofikia. Hapo ndipo limeahidiwa kuja.

114 Basi sasa tunaona kila kitu kikiwa kabisa kwenye mstari, na kujua kwamba tuko katika siku za mwisho, na ni kitu gani kilichotendeka? Shida iliingia.

115 Na yote ambayo tumemwona Yeye akifanya! Jinsi alivyonyosha nyumba zetu. Jinsi ambavyo Yeye angefanya baba na mama kuunganika tena. Mmeona hilo, mume na mke wakirudi pamoja. Amewaponya wagonjwa wenu. Wakilala hapo na kansa, wakati wengi wenu wamezileta katika chupa na jagi na sufuria. Nao madaktari wameshuhudia, wakatia sahihi taarifa; nina malundo ya hizo, na kuweka kasha lililojaa. Na hata visa vitano, vilivyoshuhudiwa, vya kufufuliwa kwa wafu, baada ya kuwa wamekufa kwa saa na saa. Vema, kuanzia... Mrefu zaidi niliojua, ulikuwa kuanzia saa tatu asubuhi moja, hadi saa tano usiku huo, karibu. Mnaona?

116 La, samahani. Mtoto mchanga huko, ambaye mama alikuwa amembeba usiku kucha mkononi mwake. Alikufa alasiri moja, akambeba usiku kucha mikononi mwake, akaja kwenye mkutano huko California. Nami nilikuwa ninaondoka alasiri hiyo. Alikuwa amefariki alasiri iliyotangulia hiyo, naye akaendesha motokaa usiku kucha, akafika kule, asingeweza kufika karibu na mahali pale. Ndipo akaweka mwili mdogo baridi mikononi mwangu, wa mtoto aliyefariki aliyekuwa amekufa siku iliyotangulia hiyo. Basi nikisimama, nimemshika mtoto huyo mchanga, na kuomba tu dua. Mwili wake mdogo ukawa na joto. Akageuka na kutazama, ndipo nikamrudishia mama yake. Kweli. Hiyo ni kweli.

117 Sasa, lakini basi tunapoona mambo hayo na kuyachunguza kikamilifu, na kutambulishwa hakika, basi ni kwa nini tunaogopa wakati shida zinapoingia?

118 Walikuwa wanatazamia...Walikuwa wameshuhudia sana kuhusu yale yaliyokuwa yamefanywa, wakasahau ni Nani aliyekuwa pamoja nao. Walikuwa wamesahau wakati huo, kwa sababu shida ziliingia.

119 Kama vile sasa, tunazo shida ambazo hatuwezi kutatua.

120 Walijaribu matanga yao, na upepo ulikuwa mkali sana, ukayapeperushia mbali. Walijaribu makasia yao, nayo mawimbi yalikuwa mazito sana yakavunjika, yakavunja makasia yao. Ndipo, wao, maskini chombo chao kiliachwa kikiyumbayumba. Labda waliufunga mkuku chini, ama ninii—ama usukani. Basi walipofanya hivyo, iliwabidi tu kukiacha kiende njia yoyote kingalienda, nacho kinarukaruka, kurashia maji.

121 Inakubidi kukabili mawimbi, katika chombo. Enyi jamaa ambao huendesha chombo mnajua kwamba huwezi kuingia moja kwa moja kwenye upepo namna hiyo, moja kwa moja kwenye wimbi. Ukifanya hivyo, utatupa chombo chako moja kwa moja chini ya bahari. Kwa hiyo inakubidi kuongoza chombo hiki, ukiache kiteremke kwa wimbi. Mawimbi yalivyotanda, unaingia moja kwa moja na kutoka pamoja nayo. Wakati wewe. . . Usipofanya hivyo, utajaza chombo chako kijae maji.

122 Vema, baada ya kila kitu kuvunjika nao wasingeweza kukishikilia zaidi, iliwabidi kukiacha tu kiyumbayumbe. Basi walipofanya hivyo, basi chombo kikajaa. Ilionekana kana kwamba matumaini yote yalikwisha. Nao hao hapo, wamefadhaika kabisa na kuogopa. Ni wakati wa jinsi gani huo uliokuwa! Ilikuwa ni shida ambayo hawangeweza kutatua tena. Ndipo basi woga ukaingia, walipogundua kwamba wasingeweza kuitatua.

123 Nasi tumeingia, vivyo hivyo, katika shida. Tumeingia katika shida ambayo sisi. . . shida za kitaifa ambazo taifa letu haliwezi kutatua. Waangalie majambazi katika taifa letu, walimpiga tu risasi Rais wetu, halafu wakaenda wakampiga risasi yule mvulana. Huo ni ujambazi tu kama jamaa yule aliyempiga risasi Rais, kwa maoni yangu, katika mauaji ya kikatili. Akiponyoka na hilo, basi wataendelea kuyafanya. Labda ataponyoka na hilo, pia. Lakini hebu angalia tu kile wafanyacho, ulimwengu wote! Kama tukimweka Abraham Lincoln katika kila parokia katika kila jimbo, wangali watafanya hivyo kwa vyovyote vile. Unaona, ni shida tusizoweza kutatua. Ja—jambo, dhambi, kutokuamini na uovu, yamenyemelea kabisa ndani yetu, yakakua karibu nasi, yakafunganisha taifa lote ndani yake.

124 Tuna shida za kanisani, mabishano, misukosuko, inaonekana kama hatuwezi kuzitatua. Tunalo sasa lile wanalojaribu kufanya, sasa wote wamekuja pamoja kwa ajili ya Baraza la Makanisa. Ha—hatuwezi kutatua hilo.

125 Tumejaribu kuleta Neno. Kristo alijaribu kurejesha Hilo kwa kujionyesha Mwenyewe, ule ufufuo, kwa miaka elfu mbili, Yeye angali ni yule yule. Waliligeuzia Hilo migongo yao, wakaondoka; wao ni wasioamini. Waaminio wa kujifanya wangali wanashikilia, kupata kosa kwenye Hilo, kadri tu wawezavyo, kuendelea na kuendelea. Lakini ni kitu gani? Ni jambo lile lile likijirudia tena.

126 Neno, wanapaswa kujua. Suluhisho kwa mambo yote lilikuwa ni nini? Ni Mungu. Katika Yohana Mtakatifu 1, inasema, "Yeye ni Neno." Tungali tuna Neno, kututoa kwenye hili. Hatuhitaji Baraza lolote la Makanisa. Hatuhitaji mafundisho haya yote ya sharti na kadhalika kuchanganywa katika Neno. Tunayo Biblia hapa, inayotuambia jinsi ya kukiendesha kitu hiki. Kurudi kwenye Biblia, kurudi kwenye

Ujumbe Wake! Huyo ni Kristo miongoni mwetu, Biblia, Biblia zilizo hai. “Nyinyi ni nyaraka zilizoandikwa,” Biblia zilizo hai, Neno la Mungu likiishi hivyo kupitia wewe! Hilo ndilo tunalohitaji.

127 Hilo ndilo lililosababisha ukomunisti kuinuka huko Urusi. Vema, wakomunisti si chama kikubwa; kuna asilimia moja tu ya Urusi ambao ni ukomunisti sasa, asilimia moja. Asilimia tisini na tisa ingali huru, lakini wao ndio wanaotawala. Wao ndio watawala. Ni kwa nini uliinuka kwanza kabisa? Kwa sababu ya uozo wa kanisa. Huo ndio uliosababisha hilo. Walichukua pesa zote kutoka kwa watu, kuleta kanisani, nao wanaishi maisha yale yale. Hawakuwa tena ila tu kama chumba chochote cha kukutania wanachama. Nao watu wakakerwa na kuchoka na hilo, na hivyo ndivyo ukomunisti ulivyozaliwa.

128 Hivyo ndivyo ulimwengu unavyozaliwa hapa. Hiyo ndiyo sababu tuna Baraza la Makanisa. Hiyo ndiyo sababu tunaingia katika muungano huu na mambo tunayofanya, ni kwa sababu kwamba wamelikataa Neno. Ni kwa nini wana mlo wa supu kanisani, kumlipa mchungaji? Kwa sababu wanaikataa njia ya Mungu, ya kulipa zaka. Hakika. Ni kwa nini wanachukua kanuni ya imani? Kwa sababu hawaitaki Biblia. Ni kwa nini wanachukua uwongo? Kwa sababu hawataki Kweli.

129 Mtu akikimbilia orofa ya chini na kufunga macho yake, aseme, “Ninakataa kusema jua linawaka.” Hakuna matumaini kwake. Lakini kama yuko tayari kutazama, jua linawaka. Akitaka kujitokeza katika hilo, afurahie baraka zake, vema. Lakini kama hataki, huwezi kufanya lolote juu ya hilo. Ungesema mtu huyo ana kasoro fulani kiakili.

130 Vema, kuna kasoro fulani ya kiroho na mtu ambaye atachukua kanuni ya imani badala ya Neno la Mungu ambalo ni kinyume na hiyo.

131 Kwenye siku ya kusulubiwa, walimtaka Barabba, mwuaji, badala ya Neno. Na leo hii wanachukua Baraza, mwuaji wa Neno, badala ya kulichukua Neno lililotambulishwa miongoni mwetu. Jambo lile lile. Hiyo ndiyo shida tuliyoingia ndani yake.

132 Sasa wanafunzi Wake wanaingia katika shida wakati mwingine, wanafunzi Wake kama wale, shida za kimwili ambazo madaktari hawawezi kutatua. Labda tuseme, “Una kansa. Imeenea.” Labda una TB iliyoenea, shida ya namna fulani. Sisi, kama wao, tunasahau Yule aliye ndani ya chombo.

133 Kulikuwa na dhoruba iliyokuja. Sasa, Mungu aliumba upepo. Mungu aliumba hewa. Mungu aliumba maji. Yote ni maumbile Yake. Aliyaumba. Bali, unaona, ilikuwa ni ibilisi aliyeingia katika hayo na kuyavuruga. Huyo ndiye huleta shida, ni ibilisi. Na sasa kama Yeye ni Muumba, na aliyafanya hivyo hapo mwanzo, hivi wanafunzi hao si wanapaswa kujua kwamba

huyo Muumba, anayelala pale, anaweza kuyafanya yakome? Amina!

134 Mungu alikuumba uwe na afya njema. Ibilisi akaingilia, hivi hufikirii kwamba itambidi kumtii Yeye, sawa na upepo? Aliufanya mwili wako. Alikufanya wewe, mwanadamu. Alikupa macho na kukupa afya. "Ningetamani, juu ya mambo yote, kwamba unawiri katika afya." Ni ibilisi ndiye huingia humo ndani. Kweli. Jambo pekee alilo tayari kufanya usiku wa leo . . . Amekuwa akipumzika kutoka kwa miamsho mingine, lakini Yeye yuko tayari kuitwa.

135 Walipaswa kujua kwamba Yeye alijua hayo yalikuwa yanaenda kufanyika.Yeye alijua mambo yote. Alijua yangefanyika. Yalikuwa tu yanathibitisha, yalithibitika kuwa tu kujaribiwa kwa imani yao. Hata ninashuku Yeye kuwa amelala. Alikuwa tu amejilaza pale nyuma. Alijua kilichokuwa kinaenda kufanyika. Naam, akingojea tu kuona kile walichokuwa wanaenda kufanya.

136 Anawasikia huko nje wakishuhudia, "Loo, utukufu kwa Mungu, tumeridhika huyo ndiye Masihi. Loo, utukufu, haleluya, tunajua hilo! Hiyo ni kweli."

Ndipo kasema, "Nitaona tu. Vema, Shetani, achilia sasa."

137 Wakaangalia huko nje, na, "Loo, matumaini yote yamekwisha! Loo, tunaenda kuangamia! Jamani, tufanye nini?" Naye Muumba Mwenyewe, walikuwa wakizungumza kumhusu, amelala pale moja kwa moja pamoja nao. Haleluya!

138 Mungu mwenyewe aliyetupatia Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu mwenyewe aliyeshuka kwenye Pentekoste, papa hapa pamoja nasi usiku wa leo; amina, Yeye yule aliyewafufua wafu, akawaponya wagonjwa; yeye yule jana, leo, na hata milele, akituthibitishia kwamba Yeye yupo hapa pamoja nasi.

139 Labda Yeye aliacha mshuko huu uje, tuite, kuja hapa ndani, ili tu kuona kile utakachofanya. Hivyo ndivyo Yeye hufanya, kuthibitisha imani yako, kuona kile utakachofanya. Kutoroka? Si Biblia inasema, "Mambo yote yatafanya kazi kwa wema kwao wanaompenda Yeye"?

140 Alikuwa amethibitisha kabisa kuwa Yeye ni Nani. Amethibitisha kabisa leo hii kuwa Yeye ni Nani, kwa kuwa Yeye amethibitisha tu kama Yeye alivyofanya wakati ule. Yeye angali ni Masihi, angali yeye yule. Yeye angali ni Neno, Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Yeye angali anatambua kama tu Yeye alivyofanya daima. Angali anaponya jinsi tu alivyofanya daima. Angali anaumba jinsi tu alivyofanya daima. Angali anawafufua wafu, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima," sawa tu na jinsi Yeye alivyowahi kuwa. Anathibitisha hilo moja kwa moja miongoni mwetu, na moja kwa moja katika chombo chetu.

141 Ndipo basi shida inaingia, na, "Matumaini yote yamekwisha." Naam, hiyo si ni—hiyo si ni kama tu wanafunzi? Hiyo ni kweli.

142 Alikuwa amethibitisha kuwa Yeye ni Nani, kwa Neno na ishara. Zilikuwa zimethibitishwa kikamilifu, kwamba Yeye alikuwa ni Yule Yeye alikuwa. Alisema, "Nisipozifanya zile kazi zilizoandikwa kunihusu Mimi, basi msiniamini Mimi. Lakini kama ninazifanya kazi zilizoandikwa kunihusu Mimi, basi aminini kwamba ninawaambia Kweli kuhusu hilo." Ni ninii—ni ninii . . . Ni jambo lile lile tulilo nalo leo hii. Alisema, "Yachunguzeni Maandiko, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

143 Walipaswa kuwa wamejua Yeye alikuwa ndiye Mungu wa maumbile yote, ambaye hata angeweza kufanya. Kama Yeye alizifanya hizo, hiyo hewa kuwepo, Yeye aliifanya dunia hii kuwepo, aliyafanya maji kuwepo; Muumba amelala pale, na kuonyesha kwamba Yeye alikuwa na uwezo juu ya hayo yote. Nao waliamini hilo, bali wakasahau kuhusu Yeye kuwepo ndani ya chombo. Kwa sababu hakuwa hapo akiwapigapiga mgongoni, wakati wote, akisema, "Sasa endeleeni, enyi wavulana, inakaribia kutukia papa hapa nje. Sasa kama ikitukia, kumbukeni tu, mimi nimesimama papa hapa karibu nanyi. Hii hapa inakuja sasa hivi, enyi wavulana, hebu tuangalie na kuona. Sasa, dakika chache tu sasa." Loo, la, Yeye hafanyi hivyo. Yeye humjaribu kila mwana na binti anayekuja Kwake, aone kama tutamwamini Yeye. Naam, bwana. Aliyaumba, hivi hayatamtii Yeye?

144 Hebu tukumbuke pia, Yeye aliiumba miili yetu, haina budi kumtii Yeye, pia. Na hiyo isingemtii Yeye? Maskini hii ninii . . .

145 Niliwaita bonge la vumbi la Texas na Louisiana. Hivyo ndivyo ulivyo, udongo. Uliinuliwa kutokana na udongo huko nje, na huko ndiko unakorudi. Unazo tu elementi kumi na sita ndani yako, unyevu kidogo, na petroli kidogo, potashi kidogo, kalisi kidogo, na nurulimwengu kidogo. Na hicho ndicho karibu ulicho, zikisokotwa pamoja, nawe huyo hapo unaenda. Vumbi ya Louisiana, hivyo tu ndivyo ulivyo. Bali, kumbuka, Kitu fulani kilikufanya huu. Na Yule hasa aliyekufanya huu, alikuja kuishi katika huu pamoja nawe, ili Yeye aweze kukufanya kitu tofauti. Loo, jamani! Loo, jinsi inavyotupasa kutazama juu ya hilo! Kumbuka, Yeye aliahidi kwamba ingawa bonge hili la vumbi lirudi kwenye . . . Bonge hili linalotembea huku likiwa na uhai ndani yake, uhai utakapoondoka, moja kwa moja ni vumbi tena.

146 Lakini Yeye alisema nini katika Neno Lake? "Nitaufufua tena katika siku za mwisho." Amina! "Nitaufufua." Aliliahidi; baada ya mwili kuangamia, baada ya hata vumbi kuvunjwa, na kurudi katika gesi za nchi. Hata hivyo, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, "Huwezi kuangamiza chochote, mwanadamu

hawezi." Hakuna maangamizi. Mwanadamu hawezi kuangamiza chochote. Ni Mungu pekee awezaye kufanya hivyo. Basi kumbuka, Yeye atafanya hivyo, ijapokuwa ni kijiko kimoja cha majivu, Yeye alisema, "Nitaufufua tena katika siku ya mwisho." Hayo mavumbi itabidi yatii amri Yake, kwa sababu Yeye aliyaumba. Kama upepo na mawimbi yanamtii Yeye, vivyo hivyo na mavumbi yanamtii Yeye. Amina.

Amkeni! Yeye yu pamoja nasi. Yote yanamtii Yeye.

147 Baada ya wa—wanafunzi kujikuta mwisho wa barabara, hapana shaka ilifunuka kwa baadhi yao, kwamba Muumba alikuwa pamoja nao. Huenda ilifunuka, kwa hiyo tunaona kwamba walienda na kumwamsha, na, kwa kuwa Yeye alikuwa pamoja nao muda wote.

148 Ndipo wakaliona Neno Lake la Kimaandiko likithibitishwa. Ndivyo na sisi. Na sisi hatujaninii. . .Tunapomwita Yesu, haikuwa vigumu. Haikuwabidi kwenda kusema, "Loo, Bwana, amka, amka! Amka! Loo, Bwana, amka, amka!" La, la.

149 Walisema tu, "Bwana!"

Kasema, "Mimi hapa."

"Si kitu Kwako kwamba tunaangamia?"

Yeye akasema, "Loo, imani yenu iko wapi, enyi wa imani haba?"

150 Jambo ndilo hilo, kusahau kwamba Yeye yu pamoja nasi; kumwita Yesu jukwaani, kutenda. Watu leo hii walisema, "Kama ningalijua hakika kwamba Huyo alikuwa ni Yeye, kama ningaliweza tu kuwa na hakika!"

151 Wangewezaje kuwa na hakika, wanafunzi walikuwaje na hakika kuhusu hilo? Sasa sikilizeni. Si kwa sababu alikuwa ni mtu mwenye elimu. Kadiri tujuavyo, Yeye hakuwa na elimu. Alikuwa tu na hekima ya Mungu. Lakini elimu ya kilimwengu, sininii. . .Hatuna kumbukumbu Yake kuwahi kwenda shule. Lakini kasisi fulani mashuhuri ama mtu fulani mashuhuri maarufu? La. La, hatuna kumbukumbu ya chochote kama hicho. Mtu wa kawaida tu. Lakini wangewezaje kujua? Sasa sikiliza kwa makini sasa, usikose hili. Wangewezaje kuwa na hakika, "Tuna hakika kwamba Wewe ndiye yule Kristo"? Wangewezaje? Kwa sababu waliona Neno lililoahidiwa likithibitishwa; kwa maneno mengine, likidhihirishwa, kufanywa lijulikane. Neno lililo hai la ahadi lilifanywa hai, likaonyeshwa moja kwa moja kupitia ule mwili, nao wakajua kwamba Mungu alikuwa ndani Yake.

152 Petro alisema, "Enyi watu wa Israeli, Judea, Yesu wa Nazareti alikuwa ni Mtu aliyethibitishwa na Mungu, miongoni mwenu, kwa yale mambo ambayo Mungu alifanya kupitia Yeye."

153 Nikodemo, yule mtu mashuhuri mwenye elimu, alikuja usiku, akasema, "Rabi, tunajua kuwa Wewe ni wa Mungu.

Mbona," kasema, "hakuna mtu angaliweza kufanya mambo hayo ufanyayo Wewe, isipokuwa Mungu awe pamoja Naye. Tunajua hilo." Lakini ni kwa nini hakulikubali? Ni kwa nini hakufanya hivyo? Unaona, lilikuwa ni kinyume na mapokeo yao. Unaona? La.

154 Naam, njia ya pekee waliyojua kwamba Yeye alikuwa, ni kwa sababu Yeye—Yeye alilifanya Neno la Mungu, lililotabiriwa kwa siku hiyo, lijiishi Lenyewe. Je! mnaelewa? Ni wangapi wanaelewa hilo vizuri, inua tu mkono wako. Unaona, Yeye alilifanya Neno lililoahidiwa la siku hiyo kuishi, ndipo walikuwa na hakika huyo alikuwa ndiye Masihi.

155 Hilo ndilo mwanamke yule alilosema, kasema, "Sasa tazama hapa, hatujakuwa na nabii kwa miaka mia nne. Nasi tunajua kwamba nabii anayefuata, atakayejitokeza jukwaani, anapaswa awe ndiye Masihi. Na huyu hapa mtu amesimama moja kwa moja hapo nje, aliyeniambia mambo ambayo nimefanya, akaniambia kwamba nilikuwa na waume watano. Na nyinyi nyote ni mashahidi wa hilo. Na Mtu huyo ameketi pale pale nje kwenye kisima cha mjini, sasa hivi. Aliniambia nilikuwa na waume watano. Si hii ndiyo ishara hasa anayopaswa kufanya Masihi? Yeye ni Neno, Mtambuzi wa mawazo yaliyo moyoni. Huyo si ni Yeye?" Hiyo ndiyo sababu watu walijua na walikuwa na hakika Yeye alikuwa Masihi.

156 Hivyo ndivyo tunavyojua Yeye ni Masihi, kwa sababu Biblia ilisema Yeye ni yule jana, leo, na hata milele, na aliahidi kufanya hili tena katika siku za mwisho.

"Vema, walimsulubisha." Naam, bali Yeye alifufuka tena.

157 Huko chini Meksiko, kisa nilichokuwa nikizungumzia, mtoto mchanga kufufuliwa, pamoja na Ndugu Moore. Waliniita huko chini kwa usaili, siku chache baada ya hapo, kanisa liliniita, waandishi wa magazeti. Wakaniambia . . .

158 Sasa kama kuna mtu mkatoliki ameketi hapa, sikutupilii sasa, kumbuka. Watu wangu ni Wakatoliki, pia. Bali, tazama, wao ni watu wazuri. Ni watu kama tulivyo sisi, wana njaa, wengi wao, na kumwonea Mungu kiu.

159 Mwandishi huyu wa habari akasema, "Hilo lilikuwa ni jambo la ajabu." Kasema, "Je! unafikiri watakatifu wetu wangeweza kufanya hilo?"

Nikasema, "Ikiwa wako hai."

Akasema, "Hawawezi kuwa mtakatifu mpaka wamekufa."

160 Nikasema, "Hivi Petro alikuwa mtakatifu kabla ya kufariki ama baada ya kufariki? Unaona? Naam. Hivi Paulo alikuwa mtakatifu kabla ya kufariki au baada ya kufariki? Alifanya jambo lilo hilo, unaona."

161 Wakasema, "Ni nini maoni yako . . . " Kasema, "Wewe ni . . . Wewe tu ni asiye-Mkatoliki, sivyo?"

Nikasema, "La, bwana. Mimi ni Mprostentanti."

Akasema, "Hupingi . . . "

Nikasema, "Mimi ninapinga, si watu, fundisho la kanisa hilo, unaona."

Ndipo akasema, akasema, "Una maoni gani kuhusu kanisa?"

Nikasema, "Nasikitika kwamba uliniuliza hilo."

Naye akasema, "Endelea na useme. Nilikuuliza."

Nikasema, "Hali ya juu ya ushirikina kuliko zote nijuazo."

Akasema, "Ushirikina?"

Nikasema, "Naam, bwana."

162 Akasema, "Ungewezaje kuliita kanisa mama, 'ushirikina'?"

Nikasema, "Ati nini mama?"

Akasema, "Kanisa mama."

163 Nikasema, "Bwana, kanisa mama la Kirumi, naam. Kanisa la kimadhehebu, yeye ni mama wa hilo. Ufunuo 17 inasema kwamba yeye yuko hivyo, 'mama wa makahaba.' Bali," nikasema, "kanisa halikuanza huko Roma. Lilianza Yerusalemu." Unaona?

Akasema, "Mungu yuko ndani ya kanisa Lake."

Nikasema, "Mungu ni Neno Lake."

164 Kwa hiyo akasema, "Nawe unasema ndilo hali ya juu kuliko yote ya ushirikina ujuayo?" Kasema, "Ungewezaje kusema hilo?"

165 Nikasema, "Chochote ambacho kinaomba wafu ni ushirikina. Wanawake hao wote, hutembea, wakiteremka barabarani kule, wakiyavuta mawe na kadhalika, wakifanya vitubio kwa mwanamke aliyekufa aliyeuawa na wapenzi wake. Na kumfanya mtakatifu, maana alifanywa mtakatifu na kanisa?" Nikasema, "Huo ni ushirikina."

Kasema, "Wewe humwomba Yesu, na Yeye alikufa."

166 Nikasema, "Bali alifufuka tena, bwana." Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Loo, jinsi mambo hayo! "Unaona, Yeye alifufuka tena." Nikasema, "Natumai sikuumiza hisia zako."

Kasema, "La, hakuna madhara yaliyofanyika."

Nikasema, "Vema." Unaona? Unaona?

167 Nini? Naam, loo, jamani, tunasahau ni Nani aliye chomboni. Unaona? "Tunawezaje kujua kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, kwa sababu kwamba hao watu wanaosema, 'sivyo ilivyo'?" Huduma Yake inaitupa moja kwa moja mikononi mwao tena. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nanyi mna hatia tu ya Damu Yake kama alivyokuwa Pilato. Iko mikononi mwenu. Hamwezi kunawa ili kuondoa Hiyo. Hivi mliwahi kuwazia hilo?

168 Ungewezaje kutamani kuwa na damu ya Rais mikononi mwako? Ungefanya nini? Unajua kinachokujia. Vema, hilo ni jambo dogo kuwa na Damu ya Yesu mikononi mwako. Hiyo ni kweli.

169 Vipi kama—kama mtu yule aliyemwua Rais. . .Labda Oswald hakumwua. Kamwe hawatajua ni nani aliyemwua, hakika. Lakini kama hakufanya hivyo, vipi kama mtu huyo yuko hai, usiku wa leo, na anajua kuwa anayo damu ya Rais mikononi mwake? Atafanya nini ikiwa watamshika na imbidi kuikabili Mahakama Kuu, haki ya taifa hili? Hebu yaangalie macho yenye hasira yakimwangalia. Unajua, angeweza kuomba rehema, aseme, "Sikumaanisha kufanya hivyo. Na—na—nawaambia, mi—mimi ni jamaa mzuri. Si—sikumaanisha kufanya hivyo." Hakutakuwako rehema. Lingekuwa jambo baya kuitazama hiyo Mahakama Kuu, namna hiyo.

170 Lakini vipi kuhusu kuangalia upande wa pili kwenye macho ya Mungu, wakati ukiwa na Damu ya Yesu Kristo, na una hatia ya kumsulubisha Yeye upya? Vipi kuhusu hilo?

171 Hivi uliwahi kuona rubani wa ndege kabla hajapanda kuingia kwenye ndege? Inambidi. . .anakagua kila chombo awezacho. Ataiweka nje ndege hiyo, atakagua kila kitu; na kusimama pale nje na kukanyaga mafuta, na kukanyaga mafuta, kuona kama itaruka, na kila kitu. Kwa nini? Yeye ana tahadhari kabisa. Anayo damu mikononi mwake asipokuwa mwangalifu.

172 Mwangalie daktari, kwa ajili ya upasuaji, jinsi anavyokagua kila kifaa, anapiga eksirei, na kila kitu. Kwa nini? Anaye mtu huyo mikononi mwake. Kama akifa, damu iko juu yake. Basi anachunguza kila kitu, kuwa na hakika kwamba damu haiko juu yake. Hiyo ni kweli. Hataki damu yoyote mikononi mwake. Damu ya mwanadamu haitaki kuwa katika mikono ya mwanadamu.

173 Lakini utafanya nini na Damu ya Yesu Kristo mikononi mwako? Sasa huwezi kuitupa Hiyo nje, useme, "Siamini Hilo." Biblia inakuhukumu. Anasema ni Yeye yule jana, leo, na hata milele; na hapa Yeye anafanya kazi, akifanya yale yale. Damu iko mikononi mwako, hata hivyo, nawe huwezi kuiosha na kuiondoa Hiyo.

174 Pilato alijaribu hilo. Kusingeweza kuwa na maji ya kutosha kuosha Hiyo na kuiondoa mikononi mwake. Alijaribu kupitisha Hiyo iendee ushirika wake, vyeo vya juu, mzee wa jimbo, kasema, "Kama utaniacha nifanye hivyo," bali ikamrudia.

175 Inarudi moja kwa moja kwako. Unaona? Huwezi kuondoa Hiyo mikononi mwako, hakuna njia yoyote ulimwenguni ila kuikubali. Njia ya pekee ya kuondolea Hiyo mikononi mwako, ni kuiweka moyoni mwako. Hiyo ndiyo njia pekee ya kufanya hiyo. Basi tunapomwona Yesu Kristo leo hii akijidhihirisha Mwenyewe hapa kama tu vile Yeye da-. . .wakati alipofanya

hapa duniani, na kuahidi kufanya hilo, tuna hakika huyu ndiye Masihi. Sasa Hiyo iko mikononi mwako, pajani mwako. Utafanya nini na huyu Yesu aitwaye Kristo?

176 Yesu alisema, "Sitakuacha. Nitakuwa pamoja nawe daima, hata kufikia mwisho wa wakati." Yeye atakuwepo vile vile tu. Tena alisema, "Sitakuacha wala sitakupungukia. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu."

177 Unasema, "Ninawezaje kuwa na hakika na hilo? Loo, Ndugu Branham, laiti ningaliweza tu kuwa na hakika!"

178 Yohana Mtakatifu 14:12, Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi naye atazifanya pia."

179 Anangojea sasa kuitwa jukwaani, kukuthibitishia hilo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, hebu twende tumwamshe Yesu, katika maisha yetu. Alikuwa hai hapa, si muda mrefu uliopita. Alikuponya wakati mmoja, Yeye alifanya *hili* na *lile*. Alikuwa hai kwako wakati huo. Yeye, Yeye yu hai usiku wa leo. Mwite Yeye jukwaani.

180 Vile tu nilivyosema, kama Shakespeare alikuwa ndani yangu ningalifanya kazi za Shakespeare. Kama Kristo yuko ndani yako, uta—utaamini Neno la Mungu kama tu Yeye alivyoamini. Alimshinda ibilisi kila wakati alipokuja; kasema, "Imeandikwa!" Hayo tu, na hayo yalisimama juu ya Hilo. Shetani alijua Yeye aliamini hilo, ndipo akamwondokea.

181 Basi, mwite Yeye alithibitishe Neno Lake, loo, jamani, ikifanya Waebrania 13:8 kweli, ndipo mashaka na hofu zitakoma kama tu vile upepo ulikoma. Upepo huo wa kale unaopitia niani mwako, "Labda sitaipata. Labda haitakuwa mimi. Labda Yeye hatafanya *hili*." Usifanye hivyo. Hakuna labda kwake. Yeye aliahidi. Hiyo inaondoa labda zote kutoka kwake.

182 "Kama ninajua Yeye alikuwa hapa!" Mbona, Yeye huyu hapa akijitambulisha Mwenyewe, vile vile tu usiku wa leo, kwa njia ile ile na ahadi ile ile kama Yeye alivyofanya wakati alipokuwa hapa duniani. Hivyo ndivyo iliwabidi wanafunzi kumwamini.

183 Imani maarufu ilikuwa, "Mtu huyo alikuwa mwendawazimu." Sasa mtu yeyote anajua hilo, sivyo, kwamba, "Mtu huyo alikuwa mwendawazimu. Naye alikuwa ni mpiga ramli wa namna fulani, pepo mwovu, Beelzebuli aliyeweza kusoma mawazo yao; namna ya roho mwovu kama upiga ramli"?

184 Yesu aliwaambia, "Huko kungekuwa ni kumkufuru Roho Mtakatifu."

185 Sasa, imeandikwa, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo naye atazifanya pia. Mimi, kama mimi . . . Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo nanyi mtapewa." Mnaona? Sasa, imeandikwa, "Kama ilivyokuwa

katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Ahadi hizi zote ambazo Yeye amekuwa akitoa! Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule, jana, na hata milele." Ahadi hizo zote, imeandikwa. Imeandikwa, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Imeandikwa, sasa hebu litendeke. Amina.

186 Mwamshe Yesu, mwite jukwaani! Je! unaogopa kufanya hivyo? Unaogopa kuichukua changamoto ya Mungu?

187 Hebu tuombe, tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu. Kila mtu kwa kicho tu uwezavyo kuwa, kwa dakika chache zijazo sasa, kamwe usisogee. Kaa tu kwa utulivu. Kama kinanda kitapigwa kwa upole, ukiweza, ninii . . . wimbo fulani.

188 Shuka chini, Bwana Yesu, uingie mioyoni mwetu, utufanye tujue udhaifu wetu.

189 "Nifinyange, Ee Bwana." Omba sasa. "Bwana Yesu, nina haja. Nifinyange na unifanye, Bwana, (mimi ni bonge dogo tu la udongo sasa) upendavyo Wewe, huku nikijitoa, loo, nikingojea, nimejitoa na ni mtulivu. Uwe na njia Yako Mwenyewe, Bwana! Uwe na njia Yako Mwenyewe!" Kote, katika jengo, kila mahali, iweni tu katika maombi ya kilindi sasa. Ninawatakeni mwombe.

Mimi towe.
Unifinyange na unifanye
Upendavyo Wewe, Huku nikingojea,
Nimejitoa na ni mtulivu.

190 Wakati wa kimya tu kabisa sasa. Omba tu, useme, "Bwana Yesu, nifanye sasa mwaminio. Ondolea mbali kutokuamini kote."

191 Ninataka kuomba kidogo kabla tu sijaitisha mstari wa maombi. Mwanangu alisema alisambaza kadi nyingi sana za maombi, alipitia kila marefu; na kila mtu, aliyehitaji kadi, alipata moja. Ninaenda kuwaombea. Tutakuwa na mstari kama tu tulivyokuwa nao hapo kabla, mstari wa mtindo wa kale, kuja hapa juu na kuomba, na kuweka mikono juu ya wagonjwa. Ninawatakeni mwamini.

192 Hivi unajisikia kama wewe unaweza kumtambua? Hivi unatambua kwamba Yeye yuko ndani ya chombo usiku wa leo? Yuko ndani ya chombo hiki kidogo, safina hii ndogo, mwili huu mdogo wa waaminio. Je! unaamini kwamba Yeye anasafiri pamoja nasi, usiku wa leo, akisafiri kwenye bahari kuu ya maisha? Ikiwa kwa kweli unaliamini kwa moyo wako wote, inua tu mkono wako, useme, "Ninaamini hilo. Ninaamini hilo. Sasa ninalikubali."

193 Baba, Wewe unaona mikono yao, wangu pamoja nayo. Ninakuamini Wewe, pia. Sasa tunangojea, Baba. Njoo, Bwana Yesu. Usiku mmoja wakati wanafunzi walifadhaishwa,

walikuwa wakizungumza na Mtu fulani, hawakujua alikuwa ni Nani. Walisema Yeye alikuwa ni Mgeni nchini. Lakini usiku mmoja, wakati walipofunga milango na Yeye akaingia ndani, Yeye alifanya jambo kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake na kufufuka Kwake. Wakajua Huyo alikuwa ni Yeye. Njoo tena usiku wa leo, Bwana, na utufanyie hayo, hivi Wewe utafanya hivyo, huku tukingojea? Tunajua tumekuona Wewe ukifanya hivyo. Pia naomba Wewe uondolee hofu zote kutoka mioyoni mwa watu.

194 Kupitia Jina la Yesu, naomba kila mmoja tunayemwekea mikono, usiku wa leo, jalia waponywe, kila mmoja wao. Jalia kusiwe na mtu mnyonge. Jalia kila mgonjwa, anayekufa, ugonjwa wa moyo, na ugonjwa wa kike, na kansa, na TB, na leukemia, chochote kiwezacho kuwa, jalia waponywe usiku wa leo, Bwana.

195 Naomba, wanapopitia mstari huu na tunawawekea mikono yetu, jalia watambue si tu kupitia tu kwa mwanadamu, bali Mungu na mwanadamu ni mmoja. Mungu ameingia ndani ya mwanadamu, na Mungu hafanyi chochote kando na mwanadamu. Hilo ndilo Yeye afanyalo. Kazi Zake ni kupitia mwanadamu. Alimfanya mwanadamu mshirika Wake.

196 Wakati Yesu aliposimama, akitazama mavuno, Yeye alisema, "Mavuno yameiva, wafanyakazi ni wachache; ombeni Bwana wa mavuno." Na Yeye alikuwa ndiye Bwana wa mavuno. Kwa maneno mengine, "Niombeni Mimi kufanya kile ninachojua kinafaa kufanywa."

197 Lakini alikuwa amejiunganisha Mwenyewe na wanafunzi Wake. Wao ndio walikuwa waombe. Alisema, "Hamna, kwa sababu hamwombi. Hamwombi, kwa sababu hamsadiki." Lakini, Baba, tunaamini, na tunaomba usiku wa leo kwa ajili ya rehema Zako kuwa pamoja nasi tena. Katika Jina la Yesu. Amina.

198 Sasa, kila mmoja wenu mkiwa na kadi zenu za maombi sasa, tutawaomba mpange mstari. Nami sijui ni wapi . . . Labda wako kwenye orofa ya juu, orofa ya chini, na mahali walipo. Tutakuwa na yapata—yapata nusu saa hapa, au zaidi, kwa ajili ya kuombea wagonjwa. Ni saa tatu tu sasa, ama labda imepita kidogo. Tunafikiri tunaweza kufanya hivyo, na tumalize.

199 Sasa tazama. Sasa mtu yeyote asiondoke. Kila mtu kaa kimya kabisa sasa. Mnataka ibada ya uponyaji, hiyo ndiyo tumekuwa tukingojea. Je! mmekuwa mkingojea ibada ya uponyaji? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, ipo hapa sasa. Naye Mponya yupo hapa, Yesu Kristo, Yeye yupo hapa.

200 Sasa, kumbukeni, vipi kama Yeye alikuwa amevaa suti hii hapa, ambayo aliwafanya wanafu- . . . mmoja wa watumishi Wake, Ndugu na Dada Collins wanaoketi huko nje, kutoka maskani yangu, kunipatia? Vipi kama—kama Yeye alikuwa

hapa amevalia suti hii, na Yeye alikuwa amesimama hapa kama tu ninavyosimama hapa sasa? Je! wajua, kama ungesema, "Bwana, naomba Wewe uniponye," je! wajua Yeye asingeweza kufanya hivyo kinyume na imani yako? Ni wangapi wanajua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ingekubidi kumwamini Yeye kama unavyoamini sasa. Hiyo ni kweli. Ingekubidi kumwamini Yeye kama unavyoamini sasa.

201 Pia kumbuka, kile ambacho amefanya tayari, Yeye hawezi kufanya tena. Mnaona, Yeye ameuweka mbali na Yeye sasa. Ameuweka mahali unapoweza kuufikia. Yeye amefanya yote awezayo kufanya. Hiyo ni kweli, wahudumu? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.] Mnaona, hakuna kitu Yeye awezacho kufanya kuhusu huo. Hauko mkononi Mwake. Uko mkononi mwako. "Kwa kuwa Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa mapigo Yake sisi tulipona." Unaona? Unaona, hauko mkononi Mwake. Upo, lakini ameuleta karibu na wewe. Uko mahali unapoweza kuufikia sasa. Uliwekwa hapo kwa ajili yako. Angeelekeza tu mahali ulipo.

202 "Vema," unasema, "Kama mimi . . . Daima limekuwa fumbo kwangu. Kama Yeye ni, kama . . . Kwa kweli, ukweli ni kwamba, je! Yeye angali hai?"

203 Hakika, Yeye yu hai. Ni kitu gani hiki unachojigonga kwacho kila mara? Ni nini hicho kinachokuhukumu wakati umekosea? Ni nini hicho kinachokufanya kuamini? Hicho ni Yeye. Huenda usiweze kuyafumbua macho yako na kumwona Yeye, kwa sababu Yeye yuko katika umbo la roho, Mungu asiyeonekana. Lakini Yeye anaishi miongoni mwa watu wanaoonekana, akijifanya Mwenyewe kuonekana kwa Neno Lake lililoahidiwa ndani ya watu hao. Mnaelewa hilo sasa?

Hapa, kabla hatujaitisha mstari wa maombi, ninatumaini Mungu atafanya hili.

204 Mimi, ninawapenda, Maskani ya Uzima. Mnajua hilo. Nimekuwa ndugu yenu. Nimejaribu kuwa hivyo, kwa vyovyote vile. Nimeshindwa mara nyingi, lakini nimejaribu kuwa hivyo.

205 Sikiliza. Jirudie, usiku wa leo. Amka, kabla haijachelewa sana. Unaona, amka, upesi. Yeye yupo hapa pamoja nasi. Sasa ninataka kila mmoja wenu . . .

206 Ninaenda, kutoka kilindi cha moyo wangu, ninaenda kujaribu kuwaita watu ninaowajua katika jengo hili, na, haijalishi nikitazama kukupita, hiyo inaonyesha kwamba ni—ninakupita; ikiwa Nuru ya—ya hii iko juu yako, nitaipita.

207 Nina hakika kabisa huyu ni Ndugu Julius Stadsklev, mke wake na familia, wanaoketi papa hapa kwenye kiti hiki cha mbele. Naam, nina hakika na hilo.

208 Na halafu mtu mwingine ninayemwona, ninayemjua. Sasa hebu kidogo tu. Nimemwona mtu fulani dakika chache

zilizopita, ambaye nilidhani nimemtambua, na huyo alikuwa ni Ndugu Evans, lakini nimepoteza mahali alipo sasa. Ndugu Welch Evans, naam, naam, samahani. Naam.

209 Na Fritzinger anayeketi moja kwa moja karibu naye. Hiyo ni familia hiyo inayoketi papa hapa. Kina Evans na kina Fritzinger wakiketi pale pamoja.

210 Na sasa hapa ni Ndugu na Dada Dauch, wameketi papa hapa. Ninawajua.

211 Pia ninamjua huyu msichana mdogo hapa, mmoja wao. Maskini June, huyo ni binti wa Ndugu Evans na Dada Evans.

212 Pia nilimsikia Fred Sothmann akisema, "Amina." Hakuna mtu asemaye hiyo kama yeye. Yeye yupo hapa ndani mahali fulani. Sijui mahali alipo. Yuko huko nyuma, mahali fulani. Uko wapi, Fred, wapi, wapi? Loo, naam, pale nyuma.

213 Na je! huyo ni Ndugu Wood anayeketi hapo karibu nawe? Naam, Ndugu Wood. Vema.

Vema, huyu ni mvulana wa kanda anayeketi hapa, Jim Maguire.

Na yule ni Ndugu Blair ameketi moja kwa moja pale.

214 Vema, nafikiri hao ndio wote ninaowaona ambao ninawajua. Sasa, huenda nimekuona. Baadhi ya nyuso zenu zinaonekana kama kwamba nimewahi kuziona, bali sijui ni nani hao. Sasa, Roho Mtakatifu anajua hilo.

215 Lakini sasa, nyinyi watu ambao mimi . . . ambao—ambao—ambao ninawajua, unajua ninakujua, sivyo, wewe ninii tu—wewe omba tu. Usiombee chochote wewe mwenyewe. Usijaribu kumgusa Yeye. Niombee tu mimi, unaona. Niombee tu, kwamba Mungu ambaye unajua kwamba ninamtumikia, kwamba Yeye aweze kumrehemu mtu mwingine anayeketi karibu. Sasa nyinyi ombeni. Na hebu tumwulize tu Yeye kama atajitambulisha Mwenyewe, Masihi.

216 Naam, ninaamini . . . Sina hakika, bali nafikiri ninamwona Dada Moore. Je! huyo ni Dada Moore? Ni—nilifikiri yeye . . . Huyo alikuwa ni yeye. Amepoteza uzito kidogo, na hiyo ndiyo sababu sikumtambua kwanza, bali nilifikiri kwamba nilimtambua ameketi moja kwa moja pale.

217 Sasa ombeni tu sasa, kila mtu kuwa tu na—na kicho kabisa. Nawe angalia ninii . . . ama uangalie chini, chochote utakacho, na uombe tu.

218 Na sasa sikiza, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa hebu nichukue Andiko hili kwa ajili ya usiku wa leo, badala ya yule mwanamke kugusa vazi Lake. Hebu tulirudishe tu nyuma kwa kile ambacho nimekuwa nikihubiri, Neno. Sasa, Biblia ilisema kwamba, "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu zaidi, kuliko upanga ukatao kuwili," hiyo ni Waebrania 4, "na Hilo

ni Mtambuzi mawazo na makusudi ya moyo na nia." Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu." Sasa, Neno ni ahadi, kwamba Neno Lenyewe ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Je! hiyo ni kweli? ["Amina."] Sasa ombeni. Hilo lingewezaje kuwa wazi zaidi?

219 Ombeni sasa, iweni tu na kicho kabisa na muombe. Pasipo kuwajua. Ninii tu, na wewe ninayekujua, mwombee mtu fulani ambaye simjui, kwamba Bwana atamgusa mtu fulani; ili waweze, kwa kugusa.

220 Sasa, upesi, ninaona Hiyo ikiinuka. Huku upande wangu wa kushoto, karibu na ukuta, mbali kabisa upande wangu wa kushoto, kuna mtu ambaye ameketi pale ambaye anaomba. Simjui. Na hiyo Nuru inaning'inia moja kwa moja juu yake. Na mtu huyo ana shida ya pafu ambayo anaombea. Amekuwa na upasuaji kadhaa kwenye hayo mapafu. Yeye ni m—mtu mwenye umri wa makamu, amevaa miwani, nywele zinaingia mvi. Naye ni. . .Je! unaamini, bwana? Mtu ninayezungumza naye, Bw. Buford. Hilo ndilo jina lako, bwana. Wewe amini sasa, Yesu Kristo atakufanya mzima kama utaamini.

221 Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu. Sasa kama mtu yeyote anataka kumwona; waweza kusimama kwa miguu yako, yeyote ambaye huyo mtu alikuwa. Simama, wapi, hapo. Haya basi. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Sasa, nini, ni nini hiyo? Koma. "Waweza kueleza hilo, Ndugu Branham?" Siwezi. Ni nani angeweza kueleza hilo? Siwezi. La.

222 Hapa, yupo mama anayeketi huko nyuma upande wa nyuma. Nami ninamwona akiomba. Na ninamwona mwanamume fulani akipepesuka, na kwa namna fulani akirusha mikono yake hewani. Anayumbayumba. Ni mume wake. Yeye ni mlevi wa pombe. Yeye hunywa pombe, wakati wote. Naye anaombea kufunguliwa kwake. Jina lake ni Bibi Morgan. Inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Mimi ni mgeni kwake, lakini hiyo ni kweli.

223 Simama, mama ambaye ndio kwanza atajwe. Huyo hapo, nami simjui mwanamke huyo. Niambie ni kitu gani alichogusa, huko nyuma. Neno ni nini? "Tambuzi, na la mawazo na makusudi ya moyo."

224 Nyinyi nyote mnaweza kukaa chini sasa, mshangilie, muwe na furaha, kama mnataka kuketi. Haiwabidi kuketi; vile tu upendavyo, chochote unachotaka kufanya. Iweni tu na furaha na mshangilie, kwa sababu Bwana amekuwa mwema kwenu.

225 Huyu hapa mama moja kwa moja hapa mbele zangu. Naye ni mgonjwa sana, labda ni mgonjwa kuliko vile anavyofikiria amekuwa nao. Kwa kweli anaugua bawasiri, na zinakuwa na kansa. Bibi Morgan. . .si Bibi Morgan, samahani. Ni Bibi Anderson. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakupa afya. Je! unaamini hilo, mama?

226 Simama kwa miguu yako, kama hiyo ni kweli. Simjui huyo mama. Yeye yuko moja kwa moja kabisa mstarini pamoja na huyu mama mwingine, na niliweza kuona hiyo ingali ikining'inia hapo. Hiyo ndiyo sababu. Hivi majuzi usiku . . . Unaweza kuketi chini, ukipenda, dada. Na uamini, nawe utaponywa.

227 Bw. Wood hapa, nilienda huko chini pamoja naye, kwa mawindo ya siku moja, huko chini Kentucky. Wakati nilipokuwa nimesimama mahali hapo, shemeji yake, si Mkristo, alikaribia, akidhania kwamba alikuwa na kansa kooni mwake. Nilikuwa nimeona ono asubuhi hiyo, la mwanamke aliyevalia gauni lenye mirabamiraba. Alikuwa na koti jekundu, na alipoingia katika chumba kingine na (sikujua ni kwa nini alikuja karibu) akavua hilo koti jekundu, akarudi, alikuwa na gauni lenye mirabamiraba. Nikasema, "Njoo hapa." Hilo lilitosha. Roho Mtakatifu alimwambia kuwa kilikuwa ni kitu gani, na hilo lilitosha. Hata haikumbidi kwenda kwa daktari. Ilikwisha.

228 Dakika chache baada ya hapo, kulikuwa na mwanamume, bila kujua ni kwa nini alikuja hapo, akifa kwa ugonjwa wa moyo. Ndipo akasema, "Je! uko na wengine?"

229 Ndipo mama huyo akasema, "Ndugu Branham yuko huko nje pamoja na Banks."

230 Akasema, "Asante kwa Mungu!" Ndipo nikaingia mle. Ameketi nyuma kitini, akifa kwa mshtuko wa moyo; Bwana alimponya. Siku mbili ama tatu baada ya hapo, kasema hakuwa amepata shida hata kidogo na huo tangu wakati ule.

231 Hapo akaja shemeji yake, akiingia, mke wa mwanawe, hasa, mwanamke mdogo, Bibi Cox. Basi kwenye maskani, siku chache kabla ya hapo, kulikuwa na mama aliyeponywa, akiwa na kisukari, aliyekuwa ameketi. Nilimwona msichana huyo akisimama katika ono. Nisingemwita, kwa sababu yeye huja huko kwenye maskani. Na siku moja ama mbili baada ya hapo, alikuwa amepelekwa kwenye kliniki akachunguzwe, naye alikuwa na kisukari kibaya. Alikuwa njiani mwake basi akirudi ili kuchunguzwa damu ya—ya—yake tena. Halafu basi ingembidi kuacha kazi, mikono yake imekufa ganzi, na kadhalika. Ndipo nikasema, "Margie, daktari anapokuchunguza, imani yako imekuponya." Nao wakampeleka kwenye kliniki, kliniki ile ile tena, wakamchunguza tena, na hicho kilikuwa kimekwisha. Kuendelea tu na kuendelea, kuendelea na kuendelea, inazidi tu kuendelea, kwa sababu Yeye ni Mungu, na Yeye hashindwi. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

232 Ninamwona mwanamume ameketi hapa, akiniangalia sasa. Amekuwa na shida kidogo maishani mwake, alikuwa na matubwitubwi wakati alipokuwa . . . Yeye kwa namna fulani ana kitu katika moyo wake. Ananiangalia moja kwa moja. Watoto wake wote ni wavulana. Anataka msichana sasa. Unajua, mwanamume huyo ni mhubiri, pia. Bw. Bird, Kasisi Bw. Bird,

inua mkono wako, bwana. Hiyo ni kweli, sivyo? Mungu anakupa haja yako, bwana. Naam.

233 Mnaona jinsi ilivyo rahisi? Mungu hukaa katika urahisi. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Akifanya kazi katika urahisi, kazi Zake kuu kufanya.

234 Umepoteza hisi yako ya kunusa, sivyo, mama? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ukiwa umeketi hapo ukiniangalia kwa uaminifu sana, ulikuwa ukiomba kwamba nikutaje. Umepata haja yako. Wewe ni mke wa mhudumu. Hiyo ni kweli. ["Ndiyo, bwana."] Umepoteza hisi yako ya kunusa. Pia una mzigo mkubwa moyoni mwako. ["Ndiyo."] Unao wana wawili ambao unawaombea. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Dada Leggs. ["Hiyo ni kweli!"] Sikuwahi kumwona maishani mwangu.

235 "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Mambo yote yanawezekana, kama unaweza kuamini." Je! mnaamini sasa Uwepo Wake upo hapa? ["Amina."] Si Yeye ndiye Mtambuzi wa mawazo, makusudi ya moyo? Yeye anajua.

236 Waulize watu hao, chunguza kote, kama yeyote anashuku. Waulize. Sijawahi kuwaona watu hao, maishani mwangu. Naam, bwana.

237 Unaamini Mungu anaweza kukuondolea hicho kivimbe? Ukiangalia kote kumwona yeye akiponywa, je! unaamini Yeye anaweza kukiponya hicho kivimbe, akupe afya? Unaamini? Mama huyu hapa karibu na wewe, pia, akiwa na uvimbe mwilini mwake, na kadhalika, unafikiri Mungu anaweza kuwapa afya, nyote wawili? Mnaamini? Vema, Yeye anaweza, kama mtaamini hilo.

238 Wewe unayeketi, ukiniangalia hapo, bwana, unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa tezi dume? Unayeketi moja kwa moja hapo nyuma umevalia tai hiyo nyeusi, unaamini kwamba Mungu atakuponya huo ugonjwa wa tezi dume? Huo ndio ulio nao. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Vema. A-ha. Mnaona?

239 Unaamini? Yeye yumo ndani ya chombo. Yeye huyu papa hapa, Neno Lake likifanya kile lilisema litafanya, kuchukua siri za moyo na kuzifanya zijulikane. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

240 Bwana Yesu, ninaziombea leso hizi zilizowekwa hapa, hawa wagonjwa na wanaoteseka. Baada ya wao kusimama hapa, Bwana, kwenye Sauti umbivu yenyewe ya Mungu ikinena kupitia wanadamu, wakati imani ikitetemesha mmoja kutoka kwa mwingine, naomba leso hizi zibarikiwe. Nao watu watakaowekewa hizo, jalia wabarikiwe na kuponywa.

241 Na sasa, Baba, wakati Roho Wako akiwa hapa, nao wanafunzi sasa, wafuasi Wako sasa wanaona kwamba Wewe

uko ndani ya chombo, hakuna haja ya kuwa na hofu. Hakuna chochote kinachoenda kudhuru chochote. Mbona, Wewe upo hapa! Wewe ndiwe Muumba. Jalia iwe hivyo, Bwana, kwamba imani yao haitashindwa wakati wakiingia kwenye mstari huu wa maombi sasa. Jalia waponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

242 Tunawezaje kuwa na hakika kwamba ni Yeye? Je! mna hakika? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tumeshawishika. Nimeshawishika kabisa kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mna hakika? ["Amina."] Nimeshawishika. Kwamba, ninajua kwamba sijui mambo hayo.

243 Sasa, vema, angalieni hapa, ninataka kuwaambieni jambo. Haya hapa ni mambo madogo tu yanayofanyika. Vipi kuhusu wale wanaoenda, walio karibu nyumbani, na huenda pamoja nami mikutanoni na kadhalika? Inueni mikono yenu, ndugu, ikiwa nyinyi nyote, na kina dada, nyinyi ambao huenda nami kwenye mkutano kote, na mambo tu ambayo hufanyika. Mbona, haya ni mambo madogo tu. Ninapowaambia mahali mbalimbali, na yale yanayoenda kufanyika hapa, "Na muwe chini *hapa*, tunaenda kukutana na mwanamume. Mnaenda kujaribu kunizuia nisimfikie. Msifanye hivyo, maana ninapaswa kwenda. Mke wake ni kitu *fulani fulani*. Anaenda kuponywa. Ninaenda kumwambia *hili*." "Mvulana huyu anavuka barabara, anaenda kuuliza jambo fulani. Nitamwambia jambo fulani; yeye atafanya *hili* na kufanya *lile*." Mbona, ni kila mara tu, wote na kila wakati, namna hiyo. Ni Yesu Kristo, si mwanadamu. Ni Kristo. Mimi ni mwanadamu, lakini Yeye ni Kristo.

244 "Ni nini karama, Ndugu Branham?" Siwezi kuieleza. Jambo la pekee nijualo, ni, kumwacha tu William Branham aondoke njiani, hivyo tu, na Yeye anachukua huu udongo na kufanya kazi kuupitia.

245 Amini hilo, je! mtaamini, Shreveport? Amini kwa moyo wako wote, na usitie shaka, utapata uponyaji wako utakapopitia hapa.

246 Sasa, maono hayakuponyi. Maono hutambulisha tu Neno Lake kuwa kweli. Unaona, umeponywa tayari. Maono huthibitisha tu kwamba Yeye yupo hapa na Yeye angali ni Neno lililo hai. Bali kwa kukuponya, hayakuponyi. Hukufanya tu ujue kwamba Yeye yupo hapa. Amekuponya tayari; Damu Yake. Sababu ya Yeye kuwa hapa ni kwamba Yeye alikuponya. Sababu ya Yeye kuwa hapa ni kuwa Yeye alikuokoa. Uhai Wake ulitolewa kwa ajili yako. Damu Yake ilimwagika. Na Yeye yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, kufanya kazi kupitia sisi, kuthibitisha kwamba Yeye yupo hapa. Lakini uponyaji wako ni kwa imani yako. Kama unaamini, ni hivyo. Amina.

247 Sasa ni wangapi upande *huu* walio na kadi za maombi, kwenye marefu haya hapa? Ninawatakeni mjitokeze kwenye marefu upande *huu*. Na punde tu wanapomalizika, basi marefu

haya hapa mjitokeze upande *ule*. Na halafu marefu *haya* hapa zungukeni moja kwa moja na kuingia moja kwa moja nyuma, na *haya* hapa, nasi tutakuja moja kwa moja katika maombi.

248 Ndugu Jack Moore, yuko wapi? [Ndugu Moore anasema, "Papa hapa."—Mh.] Je! ni—ni sawa nikiwaita wahudumu hapa juu kunisaidia? ["Ni sawa tu kabisa, ndugu."]

249 Mhudumu yeyote hapa, ambaye anauamini Ujumbe wa Bwana, ambaye anaamini kwamba Biblia imefundisha mambo haya, nawe umeshawishika kabisa kwamba Yesu Kristo yupo hapa pamoja nasi usiku wa leo, na ungetaka kuja hapa na—na kutusaidia kuweka mikono juu ya wagonjwa. Kama wewe ni . . . Kama kuna chochote maishani mwako sasa ambacho kinakuzuia usifikie imani, usije, unaona, maana inakubidi kuamini kwamba ukiweka mikono yako juu ya mtu huyu kwamba watapata afya. Unaunganisha tu imani yako na yao. Unaona ninachomaanisha? Unaunganisha imani yako na yao, kwa kuwasiliana nao, kuweka mikono yako juu yao. Na iwapo una shaka kidogo juu yake, usifanye hilo.

250 Halafu basi, tazama, kila mmoja ajaye kwenye mstari wa maombi, kama una chembe ndogo kabisa ya shaka, kwamba hutaponywa usiku wa leo, usije. Itakufanya tu kuwa mbaya zaidi. Unaona, utazidi tu kuwa mbaya, unaona, kwa hiyo usije kwenye mstari wa maombi. Ngojea mpaka kesho. Ifanye kesho wakati fulani, wakati mwingine ukiwa na imani. Usifanye hilo, kwa sababu ni kwa wale tu walio na imani ya kuamini.

251 Sasa ninawatakeni enyi ndugu wahudumu kuja hapa juu na kusimama pamoja nami huku tunapowaombea wagonjwa. Nanyi mlio jukwaani, njoni moja kwa moja chini hapa mbele sasa, moja kwa moja chini mbele ya marefu hapa, maana hatuwezi kuleta wagonjwa hao, na viti vya magurudumu na kadhalika, juu kupita marefu haya. Nitashuka chini moja kwa moja hapa na kuwaombea. Shukeni moja kwa moja hapa chini, na yeyote wenu enyi wanaume mlio hapo nyuma ambao ni wahudumu mnaoamini kwa moyo wenu wote.

252 Na sasa ni wewe, wewe ni mwaminifu, u—unahitaji kwelikweli, unaamini inaenda kutendeka. Unaona? Na halafu ikiwa unaamini, nao wanaamini; na wakati unapoweka mikono yako juu yao, jambo fulani halina budi kutukia, kama nyote wawili mtaamini hilo. Mnaona ninalomaanisha?

253 Vema, pangeni mstari moja kwa moja hapa, ndugu. Pangeni mistari miwili moja kwa moja kukingama upande *huu* sasa, kila mmoja wenu ndugu wahudumu. Laiti mngalikuja chini *huku* kidogo tu, ili waweze kuwa na hayo marefu ya kurudi nyuma, kama mtaweza, maana baadhi ya hawa huku watarudi nyuma kupitia marefu haya ya katikati. Kama mtafanya tu njia yenu moja kwa moja hapa chini, ndugu zangu, kama mtaweza. Hilo ni sawa.

254 Nafikiri inatupasa kumshukuru Bwana kwa—kwa ajili ya kundi la watu kama hawa, walio tayari kusimama machoni pa wakosoaji, chochote kile, na kuchukua msimamo wao, na kusema, "Ninaamini hilo." Amina. Ninashukuru sana kwa mtu wa namna hiyo. Nina furaha kuweka mabega yangu na yao, kuweka moyo wangu na wao, kuweka hisia yangu na yao, kuweka imani yangu na yao. Na karibu na M—Mkate wa Uzima na Neno la Mungu, sisi ni ndugu pamoja, warithi pamoja katika Ufalme pamoja na Yesu Kristo. Watu hawa huenda wasiweze kusimama na kulifanya Neno . . . Hiyo ni—hiyo ni karama, hiyo ni karama tu, ni kuonyesha ishara ya mwisho kwenye siku ya mwisho. Hilo hasa ndilo inayopaswa kufanya. Lakini watu hawa wanayo haki ile ile kuweka mikono juu ya wagonjwa, kama mtu yeyote mwingine; mimi, ama Oral Roberts, ama Tommy Hicks, ama Tommy Osborn, yeyote mwingine. Wana mamlaka yale yale, kwa Mungu yule yule, kwa sababu ni watumishi wa Mungu yuyo huyo.

255 Sasa wakati nyinyi watu . . . Ninaenda kuwa na Ndugu Price, ama mtu mwingine, ama Ndugu Moore. Unaenda kuja kutusaidia kuomba, ama unaenda kukaa kwenye . . . [Ndugu fulani anasema, "La, ninaenda kuchukua maikrofoni pale chini."—Mh.] Vema, unaenda kuchukua maikrofoni huko chini. Vema. Sasa nitakuwa na Ndugu Price. Sasa wakati tunapopitia hapa . . .

256 Sasa tazama, hebu hili liyatatue. Jambo ndilo hili. Haikubidi kumtikisa. Haikulazimu. Sema tu, "Bwana Mungu, ninaamini." Unaona, Yeye yu macho hivi sasa. Tayari amejithibitisha Mwenyewe. Ameamshwa tayari, miongoni mwenu. Ninamhisi, nami ninajua Yeye yupo hapa maana ninaona ushuhuda Wake, jinsi Yeye anavyofanya kazi. Wazia tu, Muumba Mwenyewe, Neno Mwenyewe, amewekwa dhahiri, akashuhudiwa papa hapa pamoja nasi usiku wa leo. Na kama mkichukua neno langu, inasonga tu moja kwa moja kupitia jengoni namna hiyo. Ingeweza kusimama tu hapa na kuendelea kuita, kuita, kuita, kuita. Bali, nadhani, watu wanane au kumi, ama labda zaidi, waliletwa kutoka kwenye mstari. Hilo linatosha kutambulisha kwamba Uwepo Wake upo hapa.

257 Sasa, Ndugu Price, ukipenda, ninataka kusanyiko liimbe kwa upole sana, "Tabibu mkuu sasa yu karibu, Yesu mwenye huruma." Kama Yeye alikufa ili upate afya, kwa hakika Yeye anahurumia ugonjwa wako. Yeye, Yeye anakuhurumia kwa sababu wewe ni mgonjwa. Basi wakati unapokuja kupitia mstarini, watu wa Mungu wanaenda kukuwekea mikono. Ninaenda kusimama hapa na kuchukua mahali pangu pamoja na hawa watu wa Mungu. Rudi nyuma moja kwa moja na . . .

258 Sasa, tazama, usisahau hili sasa. Fikiria sana sasa. Unapopitia kwenye mstari, iweke imani yako namna hii, "Nitakapofikia mwisho wa mstari huo, umekwisha. Ninashuka

moja kwa moja kwenye yale marefu. Nimesimama hapa, mgonjwa. Ninasimama hapa, nimefadhaika. Nimesimama hapa, mwenye hofu. Nimesimama hapa, bila kujua ni nini na nini kinachoenda kutendeka. Daktari alisema *hili*, nao walisema *hili*, na kusema . . . Lakini nitakapoenda pale chini, nitainua mikono yangu juu hewani, nikimshukuru Bwana kwamba nimepona." Halafu uangalie tu kile kinachotendeka. Sasa ningependa . . .

259 Mara nyingi, watu wana haya sana wakati unapowaangalia; watu wagonjwa, hasa. Wanakuangalia. Na, hilo ndilo, ji— ji—jicho ndilo lango la nafsi. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliwaongoza akawapeleka nje. Bila shaka, hakutakuwa na wengi watakaoponywa kwa njia hii kama vile ingekuwa kama ulikuwa nao mmoja, kwa kuwatoa nje, na kuishusha. Lakini angalia ni wangapi wanaotaka kuombewa, unaona. Huwezi kuwachukua namna hiyo. Bali sasa hii ndiyo njia ambayo imani yako haina budi kuishika.

260 Sasa, usiseme, "Mimi—mimi sijui kile, jinsi ya kulieleza hilo." Hakuna ajuaye.

261 Bali tunaliamini kwa sababu Neno lilisema hivyo. Naye Kristo aliyethibitishwa yupo hapa pamoja nasi; tumemwita Yeye jukwaani. Alifanya nini wakati tulipomwita Yeye? Alituonyesha, "Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Amina. Amini tu. Amini tu kwa moyo wako wote, wakati sisi . . . huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa.

262 Ndipo Ndugu Price, ama baadhi yao hapa wataninii . . . Ndugu Price ataelekeza mistari, na kila mmoja anapitia, na kurudi kwa kiti chako tena, tunapoimba *Tabibu Mkuu*.

263 Kisha tutaomba. Sasa hebu kila mtu, kimbele, ninataka kuomba. Maana . . . Hebu tuombe sasa. Kumbukeni, Petro, wakati alipoitwa kwenye nyumba ya Dorcas, aliomba pembeni; akasimama, akaenda na kuweka mikono yake juu ya Dorcas, na kusema, "Dorcas, simama."

264 Baba wa Mbinguni, sisi vile vile tunaomba. Wewe upo hapa. Ulijitambulisha Mwenyewe. Wewe ni Bwana wetu, Mwokozi wetu. Umetuponya mara nyingi. Katika majira haya hapa, ambapo mamia ya watu watakuwa wanakuja kutoka kwenye ile orofa ya chini na kote kila mahali, kuponywa. Watakuwa wanakuja kwenye mstari huu wa maombi. Hawa hapa watumishi Wako, sisi sote, tukiamini kwamba Wewe unaenda kufanya kile hasa ulichoahidi. Nasi tunaenda hapa kuweka mikono yetu juu ya wanaume hawa na wanawake, wavulana na wasichana, wanapopitia mstari huu. Jalia kila mmoja wao aamini, Bwana.

265 Pia tunaenda kuimba wimbo huu mtamu wa kale wa kanisa, *Tabibu Mkuu*, na huyo ni Wewe, Bwana. Sasa tunaenda nje juu ya msingi wa BWANA ASEMA HIVI. Imani yetu inatwambia, ikidunda ndani ya mioyo yetu wenyewe, kwamba

ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Na sisi ni waaminio. Tumesimama, jeshi lenye nguvu, na tunaenda kukabiliana na changamoto ya Shetani. Tunaikabili katika Jina la Yesu Kristo.

266 Vema, Ndugu Price. Na sasa kila mtu akiwa ameinamisha vichwa vyao, wakiomba, na wengine wenu mkiimba *Tabibu Mkuu*. Nao mstari wa maombi utakuwa unasonga. Ndugu Price atakuwa anaongoza wimbo huo, na kuwaelekeza watu wanapopita. Bwana awabariki sasa.

267 [Ndugu Branham na wahudumu wanawaombea wagonjwa, huku Ndugu Price na kusanyiko wakiimba, *Tabibu Mkuu*. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

268 Yesu wakati mmoja alisema, "Unajua kile nilichokufanyia?" Unaona?

269 Ni wangapi wanaoamini sasa, kwa mikono iliyowekwa juu yao, mstari ukipitia pale, kwamba hilo limefanya hasa kile Yesu alichosema litafanya? Je, mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Neno Lake haliwezi kushindwa. Kwa sababu kwamba mmesema hili, kwa sababu kwamba mmeshuhudia kwamba mnaamini hilo, ninaenda kuamini hili kwa moyo wangu wote, na kusema, "Mungu Mwenyezi anawapa afya," mnaona, maana ninajua ni Maandiko. Ni Kweli. Ninaamini kwamba kila mtu, anayepitia kwenye mstari, atakuwa mzima kabisa.

270 Sasa unafanya nini na hilo? Hulitilii shaka. Wewe lishikilie moja kwa moja mbele zako, Ishara yako. Ishara yako ni nini? Roho Mtakatifu moyoni mwako. Umepitia kwenye mstari huo, haina budi kutendeka. Hakuna njia kwa hiyo...Haijalishi ni mingapi umepitia hapo kabla, huu ndio. Hii ndiyo saa. Huu ndio wakati. Imekwisha. Imetatuliwa. Sahau tu kwamba uliwahi kuwa mgonjwa, ama kuwahi kuwa nao, kuwahi kuteseka, ama chochote. Mungu atalishughulikia kwa ajili yako. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

271 Sasa hebu tusimame, kila mmoja wetu, juu kabisa namna *hii*. Na, sasa, kama ndugu alivyosema kwenye kijitabu chake kidogo nilichosoma leo, kuinua mkono wako ni ishara ya kila mahali ya kujisalimisha. *Nasalimisha Yote*. Hebu tuuimbe.

> Natoa,
> Natoa yote,
> Yote Kwako, Kristo wangu, Mwokozi wangu,
> Natoa yote.

272 "Yesu, mimi...Mapenzi yangu, mashaka yangu, imani yangu, moyo wangu, mwili wangu, ugonjwa wangu, maisha yangu, natoa yote!"

> Kila wakati nitampenda na kumwamini Yeye,
> Katika Uwepo Wake kila siku...

273 Sasa maanisha hilo kwa moyo wako wote sasa, mnapoinua mikono yenu. “Na—natoa imani yangu, Bwana. Ninatoa yangu yote. Nimeponywa.”

Toa, natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

274 Yeye si ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, wazia, tunamaanisha hilo, kila kitu kimesalimishwa. “Mimi si mawazo yangu mwenyewe tena. Siendi kuwaza vile ningewaza, Bwana. Ninaenda tu kuwaza vile Wewe unavyowaza. Na, Wewe uliahidi kwamba niliponywa, ninawaza hilo. Ninasalimisha mawazo yangu. Sitawaza tena kuhusu ugonjwa wangu. Sitawaza kuhusu ugonjwa niliokuwa nao. Siwazi juu ya chochote bali nawaza kuhusu kile ulichosema Wewe.”

275 Sasa moja kwa moja mbele zako anasimama mtu sawa tu na ulivyokuwa dakika chache zilizopita, ulikuwa mgonjwa hapa chini, bali kuna mtu mwenye afya amesimama hapo. Yesu Kristo anamwita mtu huyo mwenye afya moja kwa moja kupita huo. Sasa wewe tu, kwa imani, unapofunga macho yako, tembea moja kwa moja kuingia ndani ya mwili huo wenye afya, unaona, halafu uendelee tu kutembea, endelea tu kusonga. “Natoa yote.” Bwana awabariki. “Na . . . ”

Nenda, Kamwamshe Yesu SWA63-1130E
(Go, Awake Jesus)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 30 Novemba, 1963, katika Maskani ya Life kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org